# KUCHUNGUZA DHAMIRA ZA KIJAMII KATIKA TAMTHILIYA YA KISWAHILI: MFANO WA TAMTHILIYA YA HATIA YA PENINA MLAMA

**ROXANA ELIAMINI MHANDO**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

# UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo **Kuchunguza Dhamira za Kijamii katika Tamthiliya ya Kiswahili: Mfano wa Tamthiliya ya *Hatia* ya Penina Mlama,** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…………………………………………….

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi)

………………………………………..

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi, **ROXANA ELIAMINI MUHANDO**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

----------------------------------------

Saini

………………………………

Tarehe

# TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wanangu wapendwa (Ester Kilela, Christine Kilela, Lucas Kilela, Leah Kilela pia mume wangu mpenzi Elias Kilela) na wazazi wangu (Mzee Eliamini Mhando na Mama Leah Mhando), bila kumsahau mlezi wangu mpendwa (mama Christine Z. Mtango) kwa kuwaeleza kuwa wasikate tamaa katika maisha kwani maisha ni mapambano. Mwenyezi Mungu awabariki wote.

# SHUKURANI

Hakuna anayestahiki kupewa shukurani wa kwanza katika dunia hii kama Mwenyezi Mungu kwa kuwa yeye ndiye atutiaye nguvu na kutuwezesha kufanya kazi zote ikiwemo hii ya tasinifu. Hivyo, ninamshukuru sana Mwanyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye Baraka tele kwa kunijalia afya na nguvu ya kutosha kuweza kufanikisha kukamilika kwa utafiti huu.

Pia, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sikumtaja na kumshukuru mwalimu na msimamizi wangu Daktari Mohamed Omary Maguo kwa kuniongoza vema katika kukamilisha kazi hii. Kazi aliyoifanya ni kubwa si tu katika kunisimamia lakini katika kunifundisha juu ya mbinu za utafiti na namna ya kufanya utafiti. Ilikuwa kazi ngumu kwangu katika kujua mbinu ipi inatumika vipi na wapi na je ni muafaka katika kutoa data zinazotakiwa? Lakini mwalimu alinifundisha vizuri na ndipo nilipofanikiwa kukamilisha kazi hii.

Pia, nawashukuru walimu wangu wote walionifundisha katika masomo ya darasani wakiwemo Prof. T.S.Y.M Sengo, Prof. E. Mbogo na Prof. J. Mdee. Wengine ni Dkt. E. Zelda, Dkt. H. Simpassa na Dkt. P. Lipembe. Nawashukuru sana walimu wangu kwa kunipatia maarifa ambayo tayari nimeshaanza kuyatumia katika kujenga taifa letu.

# IKISIRI

Mada ya utafiti huu ni kuchunguza dhamira za kijamii katika tamthiliya ya Kiswahili: Mfano wa Tamthiliya ya *Hatia* ya Penina Mlama. Katika harakati za kuishughulikia mada hii utafiti ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo ni kuelezea dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama, kutathimini uhalisia wa dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* kwa jamii ya leo ya Watanzania na kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika katika kuwasilisha dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia*. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika tamthiliya ya *Hatia* kunajitokeza dhamira za kijamii kama vile, kusema uongo katika jamii, penye ukweli uongo hujitenga, nafasi ya mwanamke katika jamii, umasikini katika jamii na matabaka katika jamii. Dhamira zote hizo zimeonekana kuwa na uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii ya Watanzania. Pamoja na dhamira hizo pia katika tamthiliya ya *Hatia* tumebaini matumizi ya mbinu mbalimbali za kisanaa katika kuwasilisha dhamira mbalimbali. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya nyimbo, takriri, tafsida na muundo wa moja kwa moja.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........................................................................................ **ii**

**HAKIMILIKI** ........................................................................................ **iii**

**TAMKO** ........................................................................................ **iv**

**TABARUKU** ........................................................................................ **v**

**SHUKURANI** ........................................................................................ **vi**

**IKISIRI** ........................................................................................ **vii**

**SURA YA KWANZA** ........................................................................................ **1**

**UTANGULIZI** ........................................................................................ **1**

1.1 Utangulizi wa Jumla ........................................................................................ 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 5

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................ 5

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ........................................................................................ 5

1.4.2 Malengo Mahususi ya Utafiti ........................................................................................ 6

1.4.3 Maswali ya Utafiti ........................................................................................ 6

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................ 6

1.6 Mipaka ya Utafiti ........................................................................................ 8

1.7 Mpango au Muundo wa Tasnifu ........................................................................................ 8

**SURA YA PILI** ........................................................................................ **9**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** .......... **9**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 9

2.2 Fani katika Tamthiliya ya Kiswahili ........................................................................................ 9

2.3 Dhamira katika Tamthiliya ya Kiswahili ........ 13

2.4 Kazi Tangulizi katika Tamthiliya za Penina Mlama ........ 14

2.5 Mkabala wa Kinadharia ........ 16

2.5.1 Nadharia ya Umarx ........ 16

2.6 Hitimisho ........ 18

**SURA YA TATU ........ 19**

**MBINU ZA UTAFITI ........ 19**

3.1 Utangulizi ........ 19

3.2 Eneo la Utafiti ........ 19

3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 19

3.4 Populesheni na Sampuli ya Utafiti ........ 20

3.5.1 Usampulishaji ........ 20

3.5 Vyanzo vya Data ........ 21

3.5.1 Data za Msingi ........ 21

3.5.2 Data za Upili ........ 21

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 22

3.6.1 Uchambuzi wa Kimaudhui ........ 22

3.6.2 Kusoma Machapisho Maktabani ........ 23

3.7 Mkabala wa Uchambuzi wa Data ........ 23

3.8 Mkabala wa Kidhamira ........ 24

3.9 Usahihi wa Mbinu za Utafiti ........ 24

3.9.1 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti ........ 25

3.9.2 Maadili ya Utafiti ........ 25

3.10 Hitimisho ........ 25

**SURA YA NNE................................................................................................27**

**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI...27**

4.1 Utanguzlizi ...........................................................................................27

4.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya Hatia .........................................................27

4.2.1 Historia Fupi ya Penina Muhando.........................................................28

4.3 Dhamira za Kijamii katika Tamthiliya ya *Hatia* ....................................29

4.3.1 Uongo katika Jamii................................................................................29

4.3.2 Penye Ukweli, Uongo Hujitenga............................................................32

4.3.3 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii ........................................................34

4.3.3.1 Mwanamke ni Mshauri Mzuri katika Jamii ........................................36

4.3.4 Umasikini katika Jamii..........................................................................38

4.3.5 Matabaka katika Jamii...........................................................................41

4.4 Muhutasari..............................................................................................44

4.5 Mbinu za Kisanaa katika Tamthiliya ya *Hatia*.......................................44

4.5.1 Matumizi ya Nyimbo katika Tamthiliya ya *Hatia* ................................45

4.5.2 Matumizi ya Takriri ..............................................................................48

4.5.3 Matumizi ya Tafsida..............................................................................51

4.5.4 Matumizi ya Muundo katika Tamthiliya ya Hatia ................................53

4.6 Hitimisho................................................................................................55

**SURA YA TANO ....................................................................................56**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.................................56**

5.1 Utangulizi...............................................................................................56

5.2 Muhtasari................................................................................................56

5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza na la Pili la Utafiti....................................56

5.2.2 Matumizi ya Mbinu za Kisanaa katika Tamthiliya Teule .............................. 57

5.3 Hitimisho .................................................................................................. 58

5.4 Mapendekezo ............................................................................................ 58

**MAREJELEO ........................................................................................................ 60**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi wa Jumla

Utafiti huu unahusu kuchunguza dhamira za kijamii katika tamthiliya ya Kiswahili kwa kurejelea tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Ili kuweza kuitendea haki mada ya utafiti wetu tumekuwa na sura hii ya kwanza ambayo imeeleza vipengele vya msingi vya kiutangulizi. Vipengele hivyo ni usuli wa utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu. Vipengele hivi vimetoa utangulizi maridhawa wa tasinifu hii ambapo msomaji anaposoma utangulizi huu anaelewa moja kwa moja tasinifu hii inahusu nini.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tamthiliya ni utanzu wa fasihi simulizi kwa asili uliokuwa ukijulikana kama natiki au maigizo unaojitokeza katika utanzu wa sanaa za maonesho (Ramadhan, 2005). Jina "tamthiliya," limekuja hivi karibuni tu katika karne ya 19 wakoloni wa Kizungu walipokuja kutawala bara la Afrika na kuleta michezo ya kuigiza ya Ulaya iliyoandikwa. Kazi hizo za awali za Wazungu zilizoingizwa katika bara la Afrika ni *Mechant of Venice* ambayo baadae ilitafsiriwa na Mwalimu Julius Nyerere na kupewa jina la *Mabepari wa Venice* (Mlama, 2003).

Kazi hii inaelezea matukio ya kipebari na athari zake katika nchi za Magharibi zikiwemo nchi za Ulaya na Marekani. Ilikuwa ni jambo la kawaida kwa wakoloni kuingiza tamthiliya na michezo ya kuigiza katika nchi za Kiafrika kwa madai kuwa

Waafrika hawakuwa na ustaarabu na hivyo kupitia kazi hizo za Wazungu Waafrika watastaarabika (Wafula, 2003).

Katika kipindi cha ukoloni, tamthiliya za Kiswahili hazikuandikwa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na mashairi na riwaya zilizoandikwa na Shaaban Robert (King'ei, 1987). Hii ilitokana na zuio la wakoloni kwa kazi za fasihi za Kiswahili kwa madai kwamba hata kama zingeandikwa, tamthiliya za Kiswahili zisingekuwa na uwezo wa kuifunza jamii ya Kiswahili ustaarabu kama ule wa Wazungu (Massoud, 2013). Mtazamo huu wa wakoloni juu ya Waswahili na Waafrika haukuwa katika tasinia ya fasihi tu bali katika mambo mbalimbali kama vile elimu, imani za dini, mila na desturi na mfumo mzima wa utamaduni wa Waafrika. Kila kitu cha Mwafrika kilionekana kuwa si lolote wala chochote mbele ya Wazungu na mila na desturi za Ulaya ndizo zilizoonekana kuwa ni bora na zinazostahiki kuigwa (Semzaba, 2003).

Jamii nyingi za Kiafrika ziliamini madai haya ya Wazungu na wengi wao kuanza kudharau mila na desturi za Kiafrika kuwa ni za kishenzi na kipumbavu na kuanza kuiga na kukumbatia mila za Kizungu (Sengo, 2009). Hata hivyo, mara baada ya kupatikana kwa uhuru katika nchi za Afrika, juhudi kubwa ilifanywa na wataalamu wa fasihi ya Kiafrika katika kuhakikisha kuwa tamthiliya za Kiswahili zinaandikwa kwa wingi kwa lengo la kuzihuisha na kuziendeleza (Mulokozi, 1996). Watunzi wa Tamthiliya katika bara la Afrika kama *Ngungi Wa Thiong'o* na *Chinua Achebe* waliandika kazi nyingi za tamthiliya zenye vionjo vya Kiafrika vya kifani na kimaudhui. Vipengele vya kifani kama wahusika, mandhari, muundo, mtindo na matumizi ya lugha katika tamthiliya hizo ni vile ambavyo vinaendana na mazingira

halisi ya jamii za Kiafrika. Waafrika wanaposoma kazi kama *Nitaolewa Nikipenda* ya Ngugi Wa Thiong'o wanailewa zaidi tamthiliya hiyo kwa sababu inazungumzia mambo yanayowahusu kupitia vionjo ambavyo wao wenyewe wanavijua (Hussein, 1983).

Katika nchi ya Tanzania pia kumekuwepo na maendeleo makubwa katika utunzi wa tamthiliya ambao zimetungwa kwa kuzingatia ujumi wa Kiafrika. Kazi hizo za tamthiliya zimetungwa na waandishi wengi lakini mwanzilishi wake ni Ebrahim Hussein na kufuatiwa na akina Penina Mhando, Amandina Lihamba, Farouk Topan, Edwin Semzaba na Emmanuel Mbogo. Ebrahim Hussein ndiye anayetajwa kama mwanzilishi na mwalimu wa tamthiliya zenye kufuata ujumi wa Kiafrika ameandika kazi kama *Mashetani*, *Wakati Ukuta*, *Alikiona*, *Kijekitile*, *Ngao ya Jadi na Jogoo Kijijini*, *Arusi* na *Kwenye Ukingo wa Thim* zikiwa zimesheheni vinjo vya Kiafrika vya kifani na kimaudhui (Msokile, 1993). Mwaifuge (2001) anaeleza kuwa, utunzi wa tamthiliya za Ebrahim Hussein umefufua tamthiliya za Kiafrika na kuleta gumzo kubwa kwa wageni waliokuwa wakidhani kuwa tamthiliya zao za Kizungu ni bora zaidi kuliko za Kiafrika. Walivutiwa na kazi za Hussein na kufanya tafiti mbalimbali katika kazi za Ebrahim Hussein na kwa namna moja au nyingine kuzikuza tamthiliya za Hussein na tamthiliya za Kiswahili kwa jumla.

Kimsingi, mmoja kati ya wanafunzi mahiri wa tamthiliya ya Kiswahili wa Profesa Ebrahim Hussein ni Penina Mhando ambaye baada ya kuolewa alijulikana kwa jina la Penina Mlama. Mtaalamu huyu naye ameandika tamthiliya za Kiswahili zenye kufuata ujumi wa Kiafrika na kuwa mmoja kati ya watunzi wa kike mashuhuri na maarufu katika tasinia ya utunzi wa tamthiliya za Kiswahili. Miongoni mwa kazi

zake za tamthiliya ni *Lina Ubani*, *Tambueni Haki Zetu*, *Pambo*, *Hatia* na *Nguzo Mama*. Uzuri wa tamthiliya hizi za Penina Mlama ni kuwa, zinawasilisha dhamira katika jamii kwa kutumia vionjo vya kifani vilivyozoeleka katika matumizi ya kila siku ya jamii ya Watanzania wakiwemo Waswahili. Wataalamu kadhaa wamevutiwa katika kuchunguza vionjo vya ujumi wa Kiafrika katika kazi za Mhando lakini hakuna aliyechunguza dhamira na uhalisia wa dhamira hizo kwa jamii kama zinavyosawiriwa katika tamthiliya ya *Hatia*.

Miongoni mwa watafiti waliochunguza kazi za Penina Mlama ni Ligembe (1995) aliyeandika tasinifu ya uzamili akichunguza matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Lina Ubani*. Kazi yake hii ilibainisha kuwa matumizi ya sitiari zinazojitokeza katika *Lina Ubani* ni zile ambazo zinatokana na vitu mbalimbali vinavyomzunguka mwanadamu kama milima, mabonde, makaazi, mashamba, mito na miti. Kutokana na hali hiyo inakuwa ni kazi rahisi zaidi kwa msomaji kuibua dhamira kutoka katika sitiari zilizojengwa kutokana na matumizi ya vitu vinavyozunguka maisha yake ya kila siku. Maaelezo haya ni ya kweli na yana mashiko yanayoweza kuaminika kitaaluma kwa sababu msomaji wa kazi za tamthiliya anapokutana na matumizi ya lugha ya sitiari ambazo zinahusiana na mazingira yake anaelewa zaidi dhamira za kazi hiyo kuliko msomaji asiyefahamu vitu na mazingira zilipotokea sitiari husika.

Hata hivyo, utafiti wa Ligembe (ameshatajwa) ulikuwa si wa kifasihi bali ni wa Kielimu mitindo kwa upande wa isimu. Tunasema hivi kwa sababu pia kuna taaluma ya elimu mitindo katika fasihi. Mtaalamu huyu alisoma shahada ya uzamili katika Isimu na si katika fasihi. Utafiti huu tulioufanya sisi ni wa kifasihi uliolenga kuchunguza dhamira katika tamthiliya ya *Hatia*.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Tamtiliya ya Kiswahili ni utanzu wa fasihi andishi ambao umekuwa na unaendelea kufanya kazi ya kuwasilisha dhamira za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi zilizo na usawiri wa hali halisi ya maisha ya Watanzania na hata nje ya Tanzania (Massoud, 2013). Tamthiliya za Penina Mhando ni miongoni mwa tamthiliya za Kiswahili ambazo zinafanya kazi kubwa ya kusawiri hali halisi ya maisha ya Watanzania kwa kutumia vionjo vya ujumi wa Kiafrika (Ligembe, 1995).

Miongoni mwa watafiti na wahakiki waliovutiwa na tamthiliya za mtunzi huyu na kuzichunguza ni Nkwera (1977), Ligembe (1995), Njogu na Chimerah (1999), Wafula (2003), Wamitila (2008), Nicholaus (2011), Massoud (2013). Kati ya watafiti hawa wote hakuna hata mmoja ambaye amechunguza dhamira kwa kina katika tamthiliya ya Penina Mlama akiwa na malengo mahususi kama ya utafiti huu tulioufanya sisi. Hivyo basi utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza kwa kina dhamira katika tamthiliya ya *Hatia* na kuelezea uhalisia wa dhamira hizo katika maisha ya leo ya jamii ya Watanzania.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahususi matatu kama yanavyowasilishwa katika sehemu ifuatayo:

#### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na mwandishi Penina Mlama.

### 1.4.2 Malengo Mahususi ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya malengo mahususi matatu ambayo ni:

(a) Kuelezea dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama.

(b) Kutathimini uhalisia wa dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* kwa jamii ya leo ya Watanzania.

(c) Kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika katika kuwasilishia dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia*.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti yanatokana na malengo mahususi. Yapo maswali matatu kama yafutavyo:

(a) Ni dhamira gani za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama?

(b) Dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* zina uhalisia gani katika jamii ya Watanzania wa leo?

(c) Ni mbinu gani za kisanaa zilizotumika katika kuwasilishia dhamira katika tamthiliya ya *Hatia*?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa katika tasinia ya taaluma za fasihi ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Kwanza kabisa utafiti huu utakuwa ni moja kati ya marejeleo ya kutumainiwa katika uhakiki na utafiti wa kazi za fasihi hususani tamthiliya. Maprofesa, madaktari na wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili watauona utafiti huu kama kichocheo cha wao kuandika makala, kufanya utafiti na kuhakiki

vipengele vya kifani na kimaudhui katika tamthiliya za Penina Mlama na watunzi wengine wa tamthiliya za Kiswahili.

Kwa upande wa wanafunzi wanaosoma shahada za awali, uzamili na uzamivu katika taaluma za fasihi watautumia utafiti huu kama sehemu ya marejeleo ya kuwasaidia kupata tatizo la utafiti na kuimarisha mapitio ya kazi tangulizi katika tafiti zao. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu utatoa chachu ya watafiti wengine zaidi kuchunguza tamthiliya za Penina Mhando na hata za watunzi wengine wa tamthiliya za Kiswahili.

Utafiti huu pia utakuwa na umuhimu mkubwa kwa watafiti wa baadae kuweza kutambua ni dhamira zipi za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya Hatia. Pia watafahamu namna uchambuzi wa data za utafiti wa kifasihi unavyofanywa kwa kutumia nadharia za uhakiki wa kifasihi. Imezoeleka katika uchambuzi wa kazi za fasihi wa kimapokeo, wachambuzi na wahakiki kutotumia nadharia katika uchambuzi wao na kufanya kazi zao kupwaya kitaaluma. Utafiti huu umetumia nadharia ya Umarx katika kuchambua data za utafiti zinazohusu dhamira na mbinu za kisanaa mtawalia.

Utafiti huu pia utakuwa na manufaa kwa watunga sera za nchi katika kukabiliana na utatuzi wa matatizo ya kijamii. Dhamira kama masuala ya elimu, matabaka, umasikini, ubaguzi wa kijinsia na kupambana na mfumo dume, umaskini na ujinga wa kutopeleka watoto shule walio na umri chini ya miaka kumi na nane ni miongoni kati ya changamoto kubwa zinazokabili jamii za Kitanzania na zimewasilishwa

vizuri katika utafiti huu. Watunga sera watakapousoma utafiti huu watachukua mbinu muafaka katika kutatua na kuondoa kero hizo katika maisha ya jamii.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Penina Mlama ameandika tamthiliya nyingi kama vile, *Tambueni Haki Zetu*, *Heshima Yangu*, *Nguzo Mama*, *Lina Ubani* na *Pambo* lakini tamthiliya ya *Hatia* inatosha kufanikisha kukamilika kwa malengo mahususi ya utafiti huu. Katika tamthiliya ya *Hatia* tumechunguza dhamira za kijamii tu licha ya kuwa katika tamthiliya hii zipo pia dhamira za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Sambamba na hilo, dhamira za kijamii zilizochambuliwa katika tasinifu hii pia zimeelezewa uhalisia wake katika jamii.

## 1.7 Mpango au Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii imeundwa katika sura sita zenye vipengele mbalimbali. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla ambapo kumefafanuliwa masuala ya msingi kama usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na hitimisho. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Kazi tangulizi zilizopitiwa ni pamoja na zile zinazohusu fani ya tamthiliya ya Kiswahili, dhamira za tamthiliya ya Kiswahili na kazi tangulizi katika tamthiliya za Penina Mhando. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti ambazo ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchambulia data. Sura ya nne inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Sura ya tano inahusu hitimisho, muhtasari na mapendekezo ya utafiti wa

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu kwa namna moja au nyingine lengo likiwa ni kubaini nini kimekwishafanywa na nini bado ili sisi tukishughulikie. Mapitio ya kazi tangulizi tuliyofanya katika sura hii yametusaidia kubainisha kuwa hakuna mtafiti hata mmoja ambaye amechambua dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia* kwa kina na kwa malengo mahususi kama ya utafiti huu.

## 2.2 Fani katika Tamthiliya ya Kiswahili

Fani ni ufundi wa kisanaa anaoutumia mwandishi katika kuisana kazi yake ili iweze kuwasilisha dhamira kwa njia inayoeleweka kwa wasomaji au wasikilizaji (Njogu na Chimerah, 1999). Fani katika kazi za fasihi ndicho kipengele kinachoifanya hadhira ya kazi husika kusema kuwa imeipenda kazi ya mtunzi au msimulizi fulani na haijaipenda kazi ya mtunzi fulani (Wamitila, 2008). Vipengele vinavyounda fani ya kazi ya fasihi ni muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Wapo watafiti kadhaa ambao wametafiti vipengele hivi katika tamthiliya mbalimbali za Kiswahili kwa nia na malengo tofautitofauti. Hivyo, katika sehemu hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi zilizotafiti vipengele vya fani ili kuoanisha na malengo ya utafiti wetu.

Hussein (1983) aliandika makala iliyokuwa imelenga kuelezea hali ya Sanaa za maonesho katika bara la Afrika na Tanzania. Anaeleza kuwa Sanaa za Maonesho

katika bara la Afrika zilikuwepo hata kabla ya ujio wa wakoloni na sanaa hizo zilisheheni fani mbalimbali. Miongoni mwa vipengele vya fani vya Sanaa za maonesho vinavyotajwa na Hussein ni pamoja na wahusika wa kifasihi simulizi, muundo, mtindo, matumizi ya lugha ya kitamathali na mandhari iliyofungamana na muktadha maalumu. Maelezo haya ya Hussein aliyatoa kana sehemu ya kukanusha hoja zilizokuwa zimetolewa na wakoloni kuwa wao ndio watu wa kwanza kuleta tamthiliya katika bara za Afrika. Kutokana na maelezo ya Hussein hapo juu inaonesha kuwa si kweli kuwa wakoloni ndio walioleta tamthiliya katika bara la Afrika.

Maelezo ya Hussein (ametajwa) yametusaidia kufahamu kuwa Sanaa za maonesho zilikuwa na matumizi ya vipengele vya fani ambavyo vilifungamana na muktadha wa jamii husika. Hii imetusukuma kuona ni kwa vipi matumizi ya mbinu za kisanaa yamesaidia katika kuwasilisha dhamira mbalimbali katika tamthiliya ya Hatia. Utafiti wetu umeeleza kwa kina matumizi hayo ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya teule ukilinganisha na makala ya Hussein (ametajwa) ambayo ilidokeza tu vipengele vya kifani katika Sanaa za maonesho.

King’ei (1987) anaeleza kuwa utunzi wa tamthiliya ya Kiswahili umekuzwa zaidi na mtunzi Ebrahim Hussein ambaye kwa makusudi maalumu ameamua kutumia fani ya majaribio katika utunzi wake wa tamthiliya. Miongoni mwa mwa vipengele vya kifani vinavyotajwa na kuwa vinatumiwa na Hussein ni uchanganyaji wa masimulizi, majaribio na ujadi katika utunzi wa tamthiliya. Matumizi ya vipengele hivi yameifanya tamthiliya ya Kiswahili kuwa mpya na yenye vionjo vya Kiafrika tofauti kabisa na tamthiliya za Kimagharibi.

Maelezo ya King'ei tunakubaliana nayo kwa kiasi kikubwa kwani Ebrahim Hussein ni mmoja kati ya waandishi wa mwanzo kabisa kuiletea tamthiliya ya Kiswahili umbo jipya kabisa la kifani. Katika kutafiti zaidi tumegundua kuwa Ebrahim Hussein ni mwalimu wa Penina Mlama ambapo kwa vyovyote vile zipo athari za kifani za utunzi wa Ebrahim Hussein zinazojitokeza katika tamthiliya za Penina Mlama ikiwemo *Hatia*. Katika utafiti wetu tumebainisha matumizi ya mbinu za kisana zenye asili ya Kiafrika katika kazi za Penina Mlama.

Ligembe (1995) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya sitiari katika tamthilia ya *Lina Ubani* ya Penina Mhando. Katika utafiti wake aligundua kwamba, matumizi ya sitiari katika tamthilia hii yapo kwa kiasi kikubwa sana na ndiyo yanayosaidia katika kujenga maudhui na dhamira mbalimbali katika kazi hiyo. Anaeleza kwamba, jina la kitabu pekee yake ni sitiari inayojitosheleza na inawasilisha maana mbalimbali ambazo zinajitokeza ndani ya kitabu chenyewe. Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa msingi kwamba, yanasaidia kuchochea utafiti wetu ambao ulilenga kutafiti dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia*. Matumizi ya jina la kitabu yanaweza kutumiwa na mwandishi kisitiari katika kujenga dhamira mbalimbali za kazi ya fasihi. Hivyo, katika utafiti wetu tulikuwa makini katika kutazama ni kwa vipi jina la kitabu linaweza kutupatia dhamira za kijamii katika tamthiliya iliyoteuliwa.

Mtafiti mwingine ambaye ameshughulikia tamthilia ya Kiswahili ni Daniel (2012) ambaye aliandika juu ya ubwege katika tamthilia ya *Amezidi*. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, tamthilia hii inaeleza ugumu wa maisha na watu kukata tamaa kwamba siku moja ugumu huo wa maisha utaondoka na wataishi maisha mazuri wao binafsi pamoja na familia zao. Hata hivyo, katika utafiti wake huu

hakuonesha ni kwa vipi dhamira hizo za kukata tamaa juu ya maisha zinazojitokeza katika tamthilia husika zinavyojengwa kwa kuwa hili halikuwa sehemu ya malengo yake kufanya hivyo. Katika utafiti wetu tulichunguza namna vipengele vya kifani vinavyohusiana na kukamilishana katika kujenga dhamira mbalimbali katika tamthilia husika. Mawazo yake tumeyachukua na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu kwa namna ambayo tayari tumekwisha ieleza.

Naye Kileo (2013) amefanya uchambuzi juu ya tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* na kubainisha dhamira mbalimbali. Miongoni mwa dhamira alizoziwasilisha ni pamoja na uongozi mbaya, ujenzi wa jamii mpya, imani za kishirikina na uchawi na nafasi ya mwanamke katika jamii kuzitaja chache. Uchambuzi huu umekuwa na manufaa makubwa katika utafiti huu kwa sababu umetuonesha kwamba katika tamthilia kuna dhamira mbalimbali zinazojitokeza na bila shaka dhamira hizi zinaweza kufanana au kutofautiana kutoka tamthilia moja na nyingine. Katika utafiti wetu tulichunguza ni kwa vipi vipengele vya kifani vinavyosaidia kujenga dhamira mbalimbali katika tamthilia iliyoteuliwa.

Pamoja na mchango mzuri wa mawazo ya Kileo (ametajwa) katika kuchochea utafiti wetu lakini bado utafiti wake unaonekana kuwa si wa kitaaluma kwa sababu ulifanywa pasipo kuongozwa na nadharia ya uhakiki wa kifasihi ili kumpatia uchambuzi makini wa dhamira katika *Kivuli Kinaishi*. Jambo hili limetufundisha na kutukumbusha kwamba matumizi ya nadharia za uhakiki wa kifasihi ni muhimu sana katika kuhakiki kazi za kifasi na vinginevyo kazi isiyotumia nadharia katika uhakiki wake basi kazi hiyo huwa inapwaya. Katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Kimarx katika kuchambua data za utafiti huu.

## 2.3 Dhamira katika Tamthiliya ya Kiswahili

Utafiti kuhusu dhamira katika tamthiliya ya Kiswahili umefanywa na wataalamu kadhaa. Miongoni mwa wataalamu waliochunguza dhamira katika tamthiliya ya Kiswahili ni Mwaifuge (2001). Mtaalamu huyu alichunguza dhamira za masuala ya imani na dini katika tamthiliya za Ebrahim Hussein kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya Uzamili katika fasihi ya Kiingereza katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa imani ya dini za Kiafrika inayohusu kuamini mizimu na miungu wengi inajitokeza kwa kiasi kikubwa katika tamthiliya za Hussein. Sambamba na hilo pia kunajitokeza imani ya dini ya Kiislamu inayoonesha kukinzana na imani na itikadi za Kiafrika.

Mawazo ya Mwaifuge (ametajwa) tunakubaliana nayo kwa asilimia mia moja kutokana na ukweli kuwa dhamira alizozitaja zinajitokeza sana katika kazi za Ebrahim Hussein. Hata hivyo, katika utafiti wake huo hakuonesha ni kwa vipi mbinu za kisanaa zimetumiwa na mwandishi katika kuibua dhamira hizo alizozitaja katika tamthiliya za Ebrahim Hussein. Utafiti wetu haukuishia katika kuchambua dhamira za kijamii peke yake katika tamthiliya zilizoteuliwa bali pia tumezama katika kuelezea mbinu za kisanaa zilizotumika katika kuwasilisha dhamira katika tamthiliya ya *Hatia*.

Mtaalamu mwingine aliyechunguza dhamira katika tamthiliya ya Kiswahili ni Wafula (2003) aliyechunguza tamthilia kwa ujumla. Katika utafiti wake ameonesha kuwa tamthiliya za majaribio zilizoandikwa na Ebrahim Hussein na Penina Mlama zimetoa dhamira ambazo zinasawiri maisha halisi ya jamii ya Watanzania kwa uhalisia usio kuwa na kasoro. Hii inatokana na ukweli kuwa tamthiliya za aina hii

zinatumia mbinu za kisanaa ambazo zinatokana na mazingira ya wanajamii na hivyo usawiri wake wa dhamira unakuwa halisia.

Kwa mfano mwandishi anaweza kuwa anazungumzia masuala ya madhara ya ukoloni katika bara la Afrika na anamtumia mhusika Shetani kumrejelea mkoloni. Bila ya shaka Shetani ni kiumbe muovu na hivyo uovu wa mkoloni unafananishwa na shetani. Hii inamfanya msomaji na mwanajamii kwa jumla kuelewa zaidi dhamira iliyolengwa ba mwandishi kuliko kama angetumiwa mhusika wa kawaida. Mawazo haya yametusaidia katika kuchambua dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia* kwa kutazama ni kwa vipi vipengele vya kifani vinaweza kujenga dhamira kwa namna rahisi yenye kueleweka kwa wasomaji.

## 2.4 Kazi Tangulizi katika Tamthiliya za Penina Mlama

Kazi za Penina Mlama zimechunguzwa na wataalamu mbalimbali kwa nia na makusudio tofautitofauti. Miongoni mwa waliochunguza kazi za mtunzi huyu ni Ligembe (1995) aliyechunguza matumizi ya Sitiari katika tamthiliya ya *Lina Ubani*. Anaeleza kuwa katika tamthiliya hiyo mwandishi amekuwa mbunifu sana katika kuunda sitiari zinazotokana na mazingira halisi ya jamii na kuifanya kazi hiyo kueleweka kwa urahisi sana kwa wasomaji wake. Mwandishi wa *Lina Ubani* ameunda sitiari zake kutokana na mito, milima, mabonde, miti na visa na matukio yanayotokea katika jamii ya Watanzania kupitia jamii ya Waluguru wa Morogoro. Sambamba na hilo, pia sitiari katika kazi hiyo zimejengwa kutokana na utamaduni wa Mwafrika.

Kazi ya Ligembe ni muhimu sana katika kufanikisha utafiti wetu kutokana na kutufahamisha moja kati ya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Penina Mlama katika

kuwasilisha dhamira za kazi zake. Ingawa sisi hatukuchunguza sitiari katika tamthiliya teule lakini tumefahamu kuwa mbinu nyingi za kisanaa katika kazi za Mlama kama tafsida, takriri na nyimbo ni vitu vinavyoundwa kutokana na mazingira ya jamii. Kwa kulielewa hili tumeweza kupata dhamira za kijamii katika riwaya teule pamoja na kubainisha mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Hatia*.

Mtaalamu mwingine ambaye amechunguza kazi za Penina Mlama ni Nicholaus (2011) aliyechunguza masuala ya Ubuntu katika kazi za mtunzi huyu maarufu. Katika utafiti huo kumebainishwa kuwa, kazi za tamthiliya za Penina Mlama zimesheheni falsafa ya Ubuntu kama inavyotumika katika kuongoza masuala mbalimbali katika maisha ya jamii. Miongoni mwa vitu vinavyoashiria kuwa katika jamii ya Waafrika kuna matumizi kuna falsafa ya Ubuntu ni ile hali ya wanajamii kuishi kwa pamoja na kindugu yaani familia pana, kula kwa pamoja, kushirikiana katika uzalishaji mali na shughuli za kijamii, kukaa katika duara wakati wa kula, kurithisha majina ya mababu kwa watoto wanaozaliwa na kuwepo kwa samani za ndani zenye umbo la duara. Maelezo haya kwa hakika ni muhimu sana katika kupeleka mbele utafiti wetu. Hii inatokana na ukweli kuwa kuzifahamu falsafa hizi kunatuwezesha kubainisha dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyotungwa na Penina Mlama.

Naye Mwita (2009) alifanya uhakiki katika tamthiliya mbalimbali za Penina Mlama akichunguza mtindo na maudhui katika tamthiliya hizo. Katika uchambuzi wake amebaini kuwa miongoni mwa dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* ni nafasi ya mwanamke katika jamii na suala la umasikini. Hata hivyo, katika uchambuzi wake hakutoa uchambuzi wa kina kwa sababu alikuwa anachambua kwa

kudokezadokeza tu dhamira mbalimbali katika tamthiliya mbalimbali za mtunzi huyu. Hivyo basi katika utafiti wetu tumechunguza kwa kina dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia*.

Kimsingi, wapo wataalamu wengine ambao wametafiti kazi za Penina Mlama kwa kina na wengine wakaishia katika kuzitaja tu katika harakati za kukamilisha malengo yao ya utafiti. Miongoni mwa wataalamu hao ni Njogu na Chimerah (1999) na Wamitila (2003; 2008). Mawazo yao yametusaidia katika kufanikisha kuibua dhamira za kijamii katika tamthiliya teule ya *Hatia*.

## 2.5 Mkabala wa Kinadharia

Katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Umarx katika kuchambua data za utafiti.

### 2.5.1 Nadharia ya Umarx

Umarx ni nadharia iliyopata umaarufu mkubwa katika tasnia ya taaluma mnamo karne ya 19 katika bara la Ulaya na baadae kusambaa duniani kote. Mwasisi wa nadharia hii ni Karl Marx aliyezaliwa mwaka 1818 huko Ujerumani na kufariki mwaka 1883 akiwa na umri wa miaka 65 (Mehring, 1962). Alisoma na kuhitimu shahada ya Uzamivu (PhD) katika Chuo Kikuu Cha Berlin mnamo mwaka 1836 na ndipo alipoanza kuandika na kuchapisha makala mbalimbali katika magazeti. Miongoni mwa mambo aliyokuwa akiyaandika ni kukosoa serikali na mfumo wa kipebari kwa misingi kwamba ulikuwa ni mfumo wa kinyonyaji kwa matajiri kuwanyonya watu maskini (Bell, 1977). Hata hivyo, hakudumu katika kuikosoa serikali na mfumo wa Kibepari alifukuzwa Ujerumani na kuhamia Ufaransa ambako nako pia alifukuzwa na kwenda kuishi London (Mehring, 1962).

Karl Marx mwanzilishi wa nadharia ya Umarx aliungwa mkono na mwanafalsafa mwingine aliyejulikana kama Fredrick Engels (Linebaugh, 1976). Nadharia ya Umarx inaeleza mambo mbalimbali lakini mawazo yake makuu ni kama yafuatayo: Karl Marx anaamini kuwa maisha ni mgongano wa kitabaka ambapo kuna tabaka la walionacho na tabaka la wasionacho. Wale walionacho ni wale wenye kumiliki nyenzo za uzalishaji mali (means of production) na wale wa tabaka la wasionacho wanamiliki nguvu ya ufanyaji kazi (lobour power).

Kuwepo kwa matabaka haya mawili kunatokea mahusiano ya kinyonyaji ambapo tabaka la wenye nacho huwanyonya watu wa tabaka la wasionacho kwa kuwafanyisha kazi nyingi kwa muda mwingi ili kujipatia faida kubwa (Marx, 1859). Maisha huendelea hivyo lakini baada ya muda watu wa tabaka la chini huchoshwa na unyonyaji na kuanza kupinga unyonyaji huo kwa migomo na njia nyingine muafaka ili kuondoa unyonyaji wa kitabaka unaofanywa dhidi yao na tabaka la walionacho (Engles, 1892). Migomo hiyo ndiyo husababisha kitu kinachoitwa “class conflict” ambacho husaidia kuleta mabadiliko katika jamii kwa kuwa ni kutokana na mgogoro wa kitabaka walionacho hubadili baadhi ya vitu na kutoa ahuweni ya maisha kwa watu wa tabaka la wasionacho (Marx, 1847).

Nadharia ya Umarx inafafanua kuwa ili kuleta usawa katika jamii ni lazima kuondosha Ubepari na kuanzisha itikadi ya Ujamaa ambayo inaitaka serikali kuwa ndiye mmiliki wa nyezo za uzalishaji mali badala ya umiliki binafsi kama ilivyo katika Ubepari. Nyenzo za uzalishaji mali zikimilikiwa na serikali zinakuwa ni mali ya umma na hivyo zitatumia kuzalisha mali ambayo itakuwa chini ya umiliki wa umma (Linebaugh, 1976). Karl Marx anaamini kuwa nyenzo za uzalishaji mali kama

ardhi, mitaji, ujasiriamali na nguvu kazi zikiwa zinamilikiwa na mtu mmojammoja kamwe haziwezi kuitoa jamii katika mfumo wa unyonyaji na hivyo kuifanya jamii kuwa na watu wengi ambao ni maskini sana na watu wachache kuwa matajiri sana (Marx na Engels, 1848). Hivyo, nyenzo za uzalishaji mali zinapomilikiwa na watu wote kupitia serikali yao upo uwezekano mkubwa wa kupunguza kama si kuondoa kabisa matabaka ya walionacho na wasionacho katika jamii.

Nadharia ya Umarx ni muafaka katika kusaidia uchambuzi data za utafiti huu uliolenga kuchunguza dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia* kwa sababu nadharia hii inahusu jamii na mgongano wa kitabaka uliopo katika jamii. Upo uhusiano mkubwa baina ya mgawanyo wa rasilimali na nyenzo za uzalishaji mali na uibukaji wa dhamira mbalimbali katika kazi ya fasihi. Hii ni sawa na kusema kuwa, umiliki wa nyenzo za uzalishaji mali na rasilimali ndivyo vitu vinavyofanya jamii ya watu fulani iwe vile ilivyo. Hivyo kwa kutumia nadharia ya Umarx tumeweza kuelezea dhamira za kijamii pamoja na matumizi ya mbinu za kisanaa zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia uliotumika katika kuchambua data za utafiti. Kazi zilizopitiwa ni zile zinazozungumzia utafiti katika tamthiliya kwa ujumla, fani katika tamthiliya, dhamira katika tamthiliya na kazi tangulizi juu ya tamthiliya za Penina Mlama. Mapitio ya kazi tangulizi katika sura hii yanaonesha kuwa hakuna mtafiti hata mmoja ambaye amechunguza na kuhakiki tamthiliya ya *Hatia* kwa kina kama ilivyofanywa katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni moja kati ya sura muhimu sana katika kuwezesha kukamilika kwa utafiti wowote ule unaokusudiwa kufanywa kwa malengo yoyote yale. Ili kuwezesha kukamilika kwa utafiti huu sura hii iliundwa na vipengele vya; eneo la utafiti, populesheni na sampuli ya utafiti, usampulishaji, vyanzo vya data za misingi na upili za utafiti na mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu. Mbinu za uchambuzi wa data zilikuwa ni mkabala wa uchambuzi wa data wa kimaelezo na mkabala wa kidhamira zilizofuatiwa na vipengele vya usahihi wa data, kuaminika kwa matokeo ya utafiti na maadili ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika jiji la Dar es Salaam ambapo Maktaba kama za Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Makavazi yake ndizo zilizotumika katika kukusanyia data za utafiti. Kimsingi, maktaba hizi zimesaidia kutupatia machapisho mbalimbali yaliyotupatia data za utafiti. Tamthilia teule ya *Hatia* ilipatikana katika maktaba hizi. Vilevile, kazi tangulizi zilipatikana katika tasinifu mbalimbali zinazopatikana katika Mataba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya East Africana pamoja na ile ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni ramani inayochorwa kuonesha sura nzima ya utafiti inavyopaswa kuwa tangu katika ukusanyaji wa data mpaka uandishi wa tasinifu

nzima (Kothari, 2008; Babie, 1999). Kuna aina mbalimbali za usanifu wa utafiti lakini katika utafiti huu tumetumia uchunguzi kifani. Uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambayo humpa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja mahususi ambalo atalichunguza kwa undani na kulitolea mahitimisho muafaka (Creswell, 2009). Good (1966) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya utafiti kwa sababu ni ya uhakika inayomuwezesha mtafiti kupata taarifa muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo ikilinganishwa na mbinu nyingine. Vile vile, uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kuuelewa muktadha mzima wa jambo analolitafiti na hivyo kuwa rahisi kwake kukamilisha malengo ya utafiti wake. Mbinu ya uchunguzi kifani inamsaidia mtafiti kujibu maswali kama vile nini? kwa nini? kwa sababu gani? Kivipi? Na kadhalika (Kothari, 2008). Utafiti wa kifasihi kama huu wetu hukusudia kujibu maswali ya aina hii. Kwa msingi huo, basi uchunguzi kifani umewezesha kukamilika kwa malengo ya utafiti wetu. Katika utafiti huu tumeteua tamthilia ya *Hatia* ambayo tumeitafiti kwa kina.

## 3.4 Populesheni na Sampuli ya Utafiti

Populesheni hurejelea idadi ya watu, na vitu ambavyo mtafiti anavitumia kama watafitiwa wa utafiti wake. Newman (2006) anaifasili populesheni kama mkusanyiko wa watu/vitu katika hali na mazingira tofauti ambavyo ndio hutoa data za utafiti husika. Populesheni ya utafiti huu ni tamthiliya ya *Hatia*.

### 3.5.1 Usampulishaji

Babbie (1999) anaeleza kwamba, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa katika populesheni kuu, ambalo ndio hutoa data za kuwakilisha kundi zima. Usampulishaji ni kitendo cha kuteua washiriki katika kundi kubwa la

watafitiwa ili kupata idadi ndogo ya watafitiwa watakaotumiwa katika kutoa data za utafiti. Utafiti huu umetumia aina ya sampuli lengwa katika kukusanya data za utafiti. Sampuli Lengwa au wakati mwingine hufahamika kama sampuli madhumuni ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteua watafitiwa wake akiwa anatambua kwamba watamsaidia kupata data anazohizihitaji ili kujibu maswali yake ya utafiti. Sampuli Lengwa ndio itakayotumika katika kupata tamthilia ya *Hatia* kwa sababu tulifahamu fika kwamba kutokana na sampuli hii ndipo tutakapopata data muafaka za kujibu maswali yetu ya utafiti.

## 3.5 Vyanzo vya Data

Utafiti huu ulikusanya data za Msingi na zile za Upili kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

### 3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni halisi na hazijawahi kukusanywa na mtafiti yeyote yule kwa madhumuni ya kujibu maswali ya utafiti yanayojibiwa katika utafiti huu. Ni data ghafi na ndio kwanza zinakusanywa kwa mara ya kwanza ili kujaza pengo la utafiti lililoachwa na watafiti tangulizi. Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kutoka katika tamthilia ya *Hatia* iliyoteuliwa katika utafiti huu.

### 3.5.2 Data za Upili

Data hizi ni zile ambazo tayari zimekwishakusanywa na watafiti wengine kwa minajili ya kujibu maswali ya utafiti wao. Data hizi zinapatikana katika vitabu, makala, majarida, tasinifu, tovuti na wavuti. Young (1984) anaieleza mbinu hii kuwa ni ya kukusanyia data mezani bila kuwatafuta/kuwafuata watafitiwa na kuwahoji

ama kuwasaili watafitiwa kuhusiana na ukusanyaji wa data katika utafiti husika. Data hizi zilikusanywa katika machapisho mbalimbali ambayo yanahusiana na mada ya utafiti huu.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti huu tumetumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui na usomaji wa machapisho maktabani katika kukusanya data za utafiti.

#### 3.6.1 Uchambuzi wa Kimaudhui

Mbinu hii hujulikana kwa lugha ya Kiingereza kama *Content Analysis*. Uchambuzi wa kimaudhui ni mbinu ambayo inampa mtafiti fursa ya kusoma andiko husika kwa utulivu na umakini kisha akaweza kubaini data ambazo zinasaidia kujibu maswali ya utafiti wake. Mtafiti aliitumia mbinu hii kukusanya data katika tamthilia ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Kothari (2008) anaeleza kwamba, Mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui ni mbinu nzuri isiyopoteza muda katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ni ya haraka hasa pale mtafiti anapotulizana na kusoma andiko husika basi huwa rahisi kumpatia data muafaka kwa minajili ya utafiti wake.

Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu hii ambapo mtafiti alisoma tamthiliya ya *Hatia* kwa kina ili kupata data zinazojibu maswali ya utafiti. Mtafiti aliandaa daftari maalumu na katika daftari hilo kulikuwa na sehemu kuu tatu ambapo sehemu ya kwanza ilikuwa inahusu data zinazohusiana na lengo la kwanza na la pili kutokana na ukaribu wa malengo hayo kimantiki. Sehemu ya pili ilikuwa inaadikwa data zinazohusiana na lengo mahususi la tatu la utafiti huu. Sehemu ya tatu ilikuwa ni kwa ajili ya kuandika data za utafiti ambazo zilionekana kuwa

zinaweza kuingia katika moja kati ya makundi hayo mawili ya data za utafiti. Hizi ni data za kati na kati ambazo zinaweza kusaidia katika kutimizwa kwa lengo kuu la utafiti.

### 3.6.2 Kusoma Machapisho Maktabani

Kusoma machapisho maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kusoma kazi tangulizi zinazohusiana na mada yake ya utafiti ili kupata data za kujazilishia data za msingi (Robson, 2007). Katika utafiti huu, mtafiti alisoma kazi tangulizi na kukusanya data za upili katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## 3.7 Mkabala wa Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizo kusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti (Young, 1984). Jambo hili liliweza kufanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo.

Mbinu hii humruhusu mtafiti kulisoma andiko fulani kwa minajili ya kulielewa katika maudhui, falsafa, mtazamo wake na mengineyo. Baada ya kuyafahamu hayo mtafiti hutumia njia ya maelezo katika kuzichambua data hizo na kuzifanya rahisi kueleweka kwa msomaji. Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ambapo maelezo ya kina yalitolewa kwa kila data ili kujibu maswali yan utafiti wetu.

## 3.8 Mkabala wa Kidhamira

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kidhamira katika uchambuzi wa data za utafiti wake. Aronson (1992) anawanukuu Taylor na Broad (1984), Benner (1985) na Leininger (1985) anasema kwamba mkabala wa kidhamira hutumika kuchambua kazi ya kifasihi kwa kutumia hatua nne. Hatua ya kwanza ni kukusanywa data, hatua ya pili ni kuoanisha data na mada ya utafiti. Hatua ya tatu ni kupangilia data, yaani kuoanisha dhamira kuu na ndogondogo. Hatua ya nne ni kutoa maelezo juu ya data zilizokusanywa ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika.

Hivyo katika utafiti huu tulizingatia hatua zote nne katika uchambuzi wa data za utafiti huu ambapo tulianza na kitendo cha kukusanya data. Baada ya hapo tulifanya kazi ya kuoanisha data za utafiti wetu na mada ya utafiti kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti wetu. Katika hatua ya tatu tulizipanga data za utafiti kwa mujibu wa mada kuu na ndogondogo ambazo zinajibu maswali ya utafiti wetu. Mada hizi kuu na ndogondogo zinaonekana katika uchambuzi wa data uliofanywa katika sura ya nne ya tasinifu hii. Hatua ya mwisho ilikuwa ni kuchambua data kwa namna maalumu inayojibu maswali ya utafiti.

## 3.9 Usahihi wa Mbinu za Utafiti

Utafiti wa kitaaluma/kisayansi hufanywa kwa kuzingatia kanuni/mbinu mbalimbali zinazokubalika ili kuufanya kuwa ni utafiti ambao hauelezi mambo ya uongo yasiyo na ukweli wa aina yoyote. Utafiti huu utatumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui, mkabala wa kidhamira na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Nadharia ya Kimarx ndio iliyoongoza utafiti huu

katika hatua mbalimbali tangu katika ukusanyaji mpaka kwenye uchambuzi wa data. Usahihi wa mbinu hizi ulijadiliwa kwa pamoja na mtafiti na msimamizi wake.

### 3.9.1 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huaminika pale ambapo taratibu zote za utafiti zimefuatwa kama ilivyoainishwa katika pendekezo la utafiti litakalowasilishwa na kujadiliwa katika semina kabla mwanafunzi hajaruhusiwa kukusanya data za utafiti wake. Utafiti huu utafuata taratibu zote muhimu zinazotakiwa mpaka kufika katika hatua hii. Mbinu zote za utafiti pamoja na nadharia zilitumiwa kama inavyopasa na pale mtafiti alipopata ugumu alikwenda kwa msimamizi wake na kufanya mashauriano mbalimbali yaliyosaidia kukamilisha kazi hii ya utafiti.

### 3.9.2 Maadili ya Utafiti

Maadili ni neno pana linalorejelea kuheshimu taratibu, miiko, mila na desturi mbalimbali katika jamii (Kumar, 1999). Utafiti kama ilivyo kwa mambo mbalimbali katika jamii una miiko yake ambayo inapaswa kuzingatiwa. Utafiti huu ulifanywa kwa misingi kwamba miiko yote ya utafiti wa maktaba inazingatiwa. Madondoo yote yaliyojitokeza katika utafiti huu yalifanywa kwa usahihi na kwamba yote yalidondolewa katika kazi zilizoteuliwa na si vinginevyo.

## 3.10 Hitimisho

Sura hii imeelezea vipengele muhimu katika kufanikisha kukusanya na kuchambua data za utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, populesheni na sampuli ya utafiti, usampulishaji na vyanzo vya data za msingi na upili katika utafiti huu. Vipengele vingine ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo ni

uchambuzi wa kimaudhui na mbinu za uchambuzi wa data ambazo ni mkabala wa kmaelezo na kidhamira. Vipengele vya usahihi wa data, kuaminika kwa matokeo ya utafiti na maadili ya utafiti pia vimewasilishwa katika utafiti huu. Kwa jumla, vipengele hivi vyote vimewezesha kupatikana kwa data za utafiti na kuzichambua data hizo kwa namna iliyosaidia kukamilika kwa malengo mahususi ya utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utanguzlizi

Katika sura hii tumefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Kombo na Tromph (2006) wanasema kuwa, kuwasilisha na kuchambua data ni kazi muhimu sana katika utafiti wowote ule wa kitaaluma kwa sababu ni kutokana na uchambuzi huo wa data ndipo matokeo ya utafiti hubainishwa na lengo kuu la utafiti kutimizwa. Hivyo katika kuwasilisha na kuchambua data za utafiti huu tumezingatia malengo mahususi ya utafiti ambayo ni kuchambua dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia*, kuelezea uhalisia wa dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* kwa jamii ya kileo ya Watanzania na kuchambua matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Kabla ya kuanza kazi ya uchambuzi wa data tumeona kuwa ipo haja ya msingi kuelezea muhutasari wa tamthiliya teule pamoja na historia fupi ya mwandishi Penina Mlama.

## 4.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya Hatia

*Hatia* ni miongoni mwa tamthiliya za zamani zilizotungwa katika kipindi cha miaka ya ishirini na tano mara baada ya uhuru wa Tanganyika. Tamthiliya hii imejihusisha na mabadiliko na maendeleo ya jamii. *Hatia* ni tamthiliya iliyotungwa na mwandishi maarufu wa tamthiliya na kazi mbalimbali za sanaa za maonyesho anayeitwa Penina Mlama. *Hatia* ni tamthiliya ya mwanzoni miongoni mwa tamthiliya na kazi nyingi za mtunzi huyu. Ilitungwa mwaka 1972 na kuchapishwa huko Kenya na East African Publishing House. Tamthiliya hii imeundwa katika maonyesho sita na wahusika

kumi na wanane. Mchezo huu umechezwa katika mandhari mbili, yaani kijijini na yale ya mjini (kijijini Kilosa na mjini Dar- es- Salaam). Matukio ya mchezo huu yamemzungukia mhusika Cheja tangu mwanzo hadi mwisho pamoja na jamii yake kwa yale aliyoyatenda ikiwa ni pamoja na kupata ujauzito na kumsingizia tajiri wake aliyeitwa Sembuli kuwa ndiye anayehusika wa mimba hiyo. Alichokusudia kukionesha mwandishi katika tamthiliya hii ni kuwa maisha ya mjini ni tofauti kabisa na maisha ya kijijini. Hivyo, mtu kama Cheja aliyetoka kijijini na kwenda mjini kutafuta maisha ni lazima awe makini sana kwa sababu mjini kuna hadaa nyingi ambazo zinaweza kumharibia maisha yake.

### 4.2.1 Historia Fupi ya Penina Muhando

Penina Mlama ni mwandishi maarufu wa tamthiliya za Kiswahili na sanaa za maonesho aliyezaliwa mwaka 1948 Mkoani Morogoro katika wilaya Kilosa nchini Tanzania na kwa sasa anakadiriwa kuwa na miaka 66. Ni miongoni mwa waandishi wanawake wa kwanza ambaye baada ya kumaliza mafunzo yake ya shahada ya kwanza mwaka 1971 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika fani ya sanaa za maonyesho (theatre arts) na ualimu, aliendelea na masomo ya elimu ya juu na kufanikiwa kutunukiwa shahada ya uzamivu ya lugha na isimu katika chuo hichohicho kwa muda mfupi tu. Penina Mlama amekuwa mwandhishi mashuhuri wa kazi za sanaa kwa utunzi binafsi na kazi nyingine akishirikiana na waandishi wengine wanawake kama akina Ndyanao Balisidya na Amandina Lihamba. Baadhi ya kazi za tamthiliya alizoziandika ni pamoja na *Hatia* (1972), *Tambueni Haki Zetu* (1973), *Heshima Yangu* (1974), *Pambo* (1975), *Nguzo Mama* (1982), *Lina Ubani* (1984) *na Talaki Si Mke Wangu* (1986). Kazi nyingine ambazo si za tamthiliya bali

ni za kitaaluma ni *Fasihi na Sanaa za Maonesho* (1976), *Abjadi Yetu* (1983) na makala mbalimbali alizozichapisha katika katika majarida ya kitaifa na kimataifa.

### 4.3 Dhamira za Kijamii katika Tamthiliya ya *Hatia*

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilihusu uchambuzi wa dhamira za kijamii katika tamthiliya ya Hatia iliyoandikwa na mtunzi Penina Mlama. Lengo hili lina uhusiano wa karibu na lengo mahususi la pili ambalo lililenga kutathimini uhalisia wa dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tahmiliya teule kwa jamii ya kileo ya Tanzania. Kutokana na ukaribu huu tumeona kuwa ni vema katika uchambuzi wa data tuunganishe malengo haya mawili pamoja ili kuleta ufanisi na tija katika kazi yetu. Inakuwa ni jambo jepesi mara baada ya kumaliza kuwasilisha na kuchambua data zinazohusu dhamira fulani ya kijamii kisha kuelezea uhalisia wa dhamira hiyo kwa jamii ya kileo.

#### 4.3.1 Uongo katika Jamii

Suala la kusema uongo katika jamii ni kitu ambacho kipo katika maisha ya kila siku katika maisha ya wanajamii licha ya kukemewa vikali katika mafundisho ya dini kupitia vitabu vyake vitukufu na hata katika mafundisho ya mila na desturi za jamii. Uongo ni kinyume na ukweli na mara nyingi inaelezwa kuwa palipo na ukweli uongo hujitenga (Nkwera, 1977). Watu katika jamii huzungumza uongo au husema maneno ya uongo ili kujinuifasha au kuwanufaisha watu fulani kwa sababu ambazo wao wenyewe wanazijua vizuri. Katika mafundisho ya dini ya Kiislamu kwa mfano, inaelezwa kuwa kusema uongo ni haramu hata kama ni mzaha (Sengo, 2009). Hii inatokana na ukweli kuwa kusema uongo kunaweza kusababisha madhara makubwa katika jamii na wakati mwingine hupelekea kupoka na kugandamiza haki za watu

wengine. Hata hivyo, katika jamii ya leo imeonekana kuwa kusema uongo ni jambo la kawaida na baadhi ya watu hunufaika nalo huku wengi wakiathirika nalo.

Katika tamthiliya ya *Hatia* mwandishi Penina Mlama anawasilisha dhamira ya kusema uongo na madhara yake katika jamii. Katika kuwasilisha dhamira hii anawatumia wahusika Cheja na Juma kuunda uongo mtakatifu dhidi ya Sembuli pale asemapo:

> CHEJA: (Polepole) Juma yale mambo ya siku ile nina mimba.
>
> JUMA: Una mimba? Yangu mimi? (Ananyamaza kama hakusikia kitu)
>
> CHEJA: Sasa tupange la kufanya. Juma usijifanye kama hujui.
>
> JUMA: Haya panga basi, panga, unasema tupange na nani? Haa! Una maana upange na mimi, tafadhali sana dada tusiingiliane, yanakuhusu wewe mwenyewe...
>
> JUMA: Aaa (kwa uovu) hiyo ndiyo shida yako? Waambie kuwa kosa hilo limetendwa na mwajiri wako.
>
> CHEJA: Kaa! (huku ameshtuka).
>
> JUMA: Ingawaje ana mke na watoto ila hutokea kwa hiyo wataamini tu (uk.08-09).

Katika dondoo hili kunaonesha namna mhusika Cheja alivyoshirikiana na Juma kuunda uongo dhaidi ya Sembuli kuwa ndiye aliyempatia Cheja ujauzito na ukweli wa mambo ukiwa sio huo. Maneno katika dondoo hilo hapo juu yanaonesha kuwa Juma ndiye aliyempatia Cheja ujauzito lakini hapa mambo yamebadilika na kuonekana kuwa Sembuli aliyempatia Cheja hifadhi ya kukaa nyumbani kwake ndiye mwenye mimba hiyo. Waswahili wanao msemo wao usemo shukurani ya

Punda ni mateke, na huo ndio ukweli wa mambo kama unavyosawiriwa na Cheja dhidi ya Sembuli. Dondoo hili linaonesha kuwa Juma ni mtaalamu wa kuunda uongo ambao unafanana na ukweli hasa pale anaposema kuwa, "ingawaje ana mke na watoto ile hutokea kwa hiyo wataamini tu." Hii ina maana kuwa mwanamume kutoka nje ya ndoa yake ni jambo la kawaida katika jamii na kwamba hakuna mtu ambaye atapinga maneno ya Cheja kuwa aliyempatia ujauzito ni Sembuli.

Kimsingi, kusema uongo ni jambo ambalo lina uhalisia katika jamii ambapo siku hizi udanganyifu umekuwa mwingi si katika mambo kama hayo ya Cheja dhidi ya Sembuli tu bali pia katika masuala ya uchumi, siasa, biashara na hata katika mahusiano. Sababu za wanajamii kusema uongo ni nyingi lakini kubwa kuliko yote ni ili kujipatia fedha au utajiri. Mwanamke anaweza kumpenda mwanamme kwa sababu tu ya mali yake lakini mali inapotoweka mwanamke huyo huondoka na kumuacha mwanamme huyo. Marx (1859) anaeleza kuwa sera za Kibepari ndizo hasa zinazosababisha watu wengi kusema uongo ili waweze kupata utajiri na kujilimbikizia mali binafsi. Kwa mfano, mfanyabiasha mkubwa anaweza kukwepa kulipa kodi kutokana na kusema uongo juu ya faida aliyoipata kutokana na biashara yake na hivyo kuipotezea serikali mapato na kuendeleza matabaka katika jamii.

Hivyo, katika malezo ya Cheja kuwa Sembuli ndiye aliyemtia ujauzito haikuwekwa bayana kuwa hasa lengo lilikuwa ni ili kumponya Juma au ilikuwa ni kupata fedha kutoka kwa Sembuli. Kwa maoni yetu tunaona kuwa upo uwezekano kuwa Juma alimshauri Cheja aseme uongo huo ili waweze kupata fedha kutoka kwa Sembuli kwa ajili ya kuendeshea maisha yao. Hii ni moja kati ya mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa na vijana wa mjini kwa nia ya kujipatia fedha kutoka kwa matajiri ili

kujinufaisha wao binafsi. Mfano mzuri unapatikana pia katika riwaya ya *Usiku Utakapokwisha* na *Kiu*.

### 4.3.2 Penye Ukweli, Uongo Hujitenga

Hii ni methali ya Kiswahili inayotumiwa na jamii kuonesha kuwa uongo daima si kitu cha kudumu bali ukweli ndio hudumu milele. Ikiwa mtu amesema uongo na ukweli ukibainika basi uongo ule hujifuta na ukweli ndio unaotamalaki. Fedheha ya kusema uongo huwa ni aibu pale ukweli unapofahamika. Katika tamthiliya ya *Hatia* mwandishi anatuonesha kuwa si vyema kusema uongo kwani ukweli ukishafahamika, aibu humrejea yule aliyesema uongo. Mhusika Cheja alidanganywa na Juma amtaje Sembuli kuwa ndiye aliyempa ujauzito kitu ambacho hakikuwa na ukweli wowote na hapa Cheja anathibitisha:

> CHEJA: Acha waje wanipige na mimi. Hata kama wakiniua sijali kwa vile sina faida kuendelea kuishi. Kaka, baba yangu wamepigwa na kuumizwa. Vile vile, Bwana Sembuli naye ameumizwa. Wote hawa kwa ajili yangu … Nitathubutuje kuwaeleza kuwa hata mmoja kati yao si mwenye hatia? Mwenyewe Juma Bakari katulia Dalisalama hana wasiwasi (uk.30).

Hapa tunaoneshwa kuwa aliyemtia mimba Cheja ni Juma Bakari lakini tayari amemzingizia mimba hiyo bwana Sembuli. Sasa umefika wakati wa kusema ukweli na uongo utajitenga tu lakini Cheja anajishauri kuwa ataanzia wapi katika kusema ukweli wa mambo? Hakuna namna ukweli ni lazima usemwe ndipo hapa Cheja anaposema:

> CHEJA: Ninachosema mwacheni. Iliyobaki naomba mnisamehe. Mnisamehe wazee Wangu, hasa Mzee Sembuli … (uk.38).

Cheja anakiri kuwa alimsingizia Mzee Sembuli kuwa ndiye aliyempatia mimba kuwa si kweli na anaomba asamehewe. Anaomba msamaha kwa wazee wote wakiwemo wazazi wake pamoja na Sembuli. Tukio hili la kuomba msamaha linaonekana kuwa na uhalisia katika jamii kwani mara nyingi watoto wanapowakosea wazazi wao huwaomba msamaha na hata watu wazima wenyewe kwa wenyewe hukuseana na kuombana msamaha ili kumaliza mambo na kurejea katika maisha ya amani na utulivu.

Imezoeleka katika jamii kuona kuwa watoto na wanawake ndio huomba msamaha lakini watu wanaume ni wagumu sana katika kuomba msamaha hata kama wao ni wakosaji. Hii inatokana na mfumo dume ambao upo katika jamii unaomkweza zaidi mwanamme na kumdunisha mwanamke (Ramadhani, 2013). Hali hii inafaa ikomeshwe kwani hakuna binadamu ambaye ni mkamilifu awe mwanamme au mwanamke na hivyo kila anayemkosea mwenzake ni vyema kuombana msamaha ili waendelee kuishi kwa amani na utulivu.

Dondoo lililopo hapo juu linatuthibitishia kuwa penye ukweli uongo hujitenga pale ambapo Cheja ameomba msamaha kwa kumtaja mhusika halisi aliyempa ujauzito tayari uongo dhidi ya Sembuli umejitenga. Jambo hili linawataka wanajamii kuhakikisha kuwa wanazungumza maneno ya kweli na si uongo kwani uongo ni mbaya na unaweza kusababisha watu kutoelewana na kuleta migogoro isiyokuwa ya lazima katika jamii. Tayari kulikwishakuwa na mgogoro mkubwa baina ya Sembuli na Cheja, Sembuli na familia ya akina Cheja na mgogoro baina ya Sembuli na jamii nzima kuwa yeye ni mtu mbaya tena mharibifu katika jamii. Mara tu baada ya ukweli kudhihirika mara moja migogoro yote hii imefutika na ukweli umesimama.

### 4.3.3 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Nafasi ya mwanamke katika jamii ni dhamira mardudi inayojitokeza sana katika kazi za fasihi bila ya kujali utanzu au kipera cha fasihi iwe simulizi au andishi (Khalifan, 2013). Tunaposema dhamira hii ni mardudi tuna maana kuwa ni dhamira inayojitokeza sana katika jamii kutokana na nafasi kubwa aliyonayo mwanamke katika maisha ya kila siku ya jamii. Mwanamke katika jamii ni mama na mlezi wa familia, mzalishaji mali katika mashamba hasa sehemu za vijijini, mjasiriamali mdogomdogo katika maeneo ya mijini na mtumishi wa masuala yote ya ndani ya nyumba ikiwa ni pamoja na usafi, kupika chakula, kumlea mume, kufua nguo, kuosha vyombo na kazi nyingi nyinginezo (Koda, 2000). Kutokana na majukumu yote haya aliyonayo mwanamke ndio maana inakuwa ni vigumu kwa kazi za fasihi kukosa kumsawiri mwanamke aidha katika hali hasi au chanya katika kazi zao.

Katika tanthiliya ya *Hatia* mwanamke amesawiriwa katika nafasi mbalimbali ikiwemo ile ya kuwa yeye ni kitega uchumi katika jamii. Mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe ambaye anaweza kuiletea familia yake utajiri wa mali nyingi kutokana na njia mbalimbali. Mwandishi anasema:

> Mzee Chimaisi: Haya sasa basi kama alivyokuwa akisema mzee mwezetu hapo mwanzo, adhabu ya Sembuli ni malipo. Na kama ilivyo jadi yetu malipo yenyewe ni sehemu tatu kwa vile ametumia nguvu. Kwanza malipo ya wazazi, pili, malipo ya msichana mwenyewe, na tatu malipo ya kumtunza mtoto atakapozaliwa. Sasa basi tuanze malipo ya wazazi.
>
> MKAMI: (kwa haraka) Ng’ombe saba, mbuzi tisa na kuku watatu.
>
> WOTE: Kaaaa! (Wanacheka.)

MZEE CHIMAISI: (huku anacheka) Babu vipi? Unataka ujipatie ng'ombe wa kuolea hapo hapo?

MKAMI: ndio, kwanza huyu dada yangu angeolewa vizuri angepata zaidi ya hizo. Sasa yeye kajitia kumharibu basi lazima alipe. Kwanza yeye tajiri. Mtu ana hata gari (uk.18).

Katika dondoo hili kunatajwa adhabu ya faini aliyotakiwa kulipa Sembuli kutokana na tuhuma zinazomkabili kuwa alimbaka Cheja na kumsababishia ujauzito. Adhabu ya faini inayotajwa katika dondoo hili ni kuwa Sembuli anatakiwa kutoa ng'ombe saba, mbuzi tisa na kuku watatu. Katika hali ya kawaida faini hii ni kubwa sana ambayo inaweza kumfanya mtu aliyekuwa hohehahe kubadili maisha yake mara moja na kuwa katika hali nzuri ya kimaisha. Hata hivyo, inaonesha kuwa mali hiyo itakayotolewa haitakuwa na manufaa kwa muathirika wa kitendo cha kubakwa bali watu wengine kama akina mkami na wazazi wa Cheja (Mwita, 2009). Maneno ya Mkami katika dondoo lililopo hapo juu yanaonesha kuwa mwanamke ni kitegauchumi na kwamba hata kama dada yake ambaye ni Cheja angeolewa ingepatikana mahari kubwa ya kutosha ya kumwezesha yeye Mkami kuoelea.

Mawazo ya Mkami kuwa mwanamke ni kitega uchumi katika jamii yanao uhalisia wa kikwelikweli katika maisha ya kila siku ya jamii. Wazazi na ndugu wa binti aliyefikia umri wa kuoa au kuolewa huwa na matarajio ya kupata mali nyingi kutoka na mahari itakayotolewa kwa ajili ya binti yao (Beyanga, 2014). Katika jamii ya Washibi wa mkoani Kagera kwa mfano, muoaji hutakiwa kutoa mahari ya hata zaidi ya ng'ombe kumi na kuendelea ndipo aweze kupewa mke (Beyanga, ametajwa). Hata hivyo, mahari hiyo inayotolewa kwa kiasi kikubwa huwanufaisha wazazi na hata baadhi ya ndugu kuliko mwanamke mwenyewe.

Suala la mwanamke kufanyiwa vitendo vya kikatili kama kubakwa na wazazi kudai fidia kubwa kutoka kwa mbakaji ni la kawaida katika jamii. Katika hali ya kawaida mbakaji alipaswa kuchukuliwa hatua za kupelekwa mahakamani ili haki iweze kutendeka. Lakini mambo huwa kinyume pale ambapo makosa ya ubakaji na mengine kama hayo hujadiliwa nyumbani na kumalizwa kwa mujibu wa mila na desturi za jamii husika. Suala kama hilo la ubakaji huzungumzwa katika mazingira ya nyumbani na kumalizika kwa mkosaji kutakiwa kutoa faini ambayo huwa haina faida yoyote kwa aliyeathiriwa na kitendo hicho. Hii ndio kumfanya mwanamke kuwa ni kitega uchumi cha wanaume katika familia. Baba na watoto wa kiume kama Mkami ndio hunufaika zaidi na mahari au faini wanazotozwa watu waliowafanyia mabaya wanawake katika jamii. Haya ni mazao ya mfumo dume unaoendelea kutawala katika jamii na bila ya kukomeshwa wanawake wataendelea kuwa katika tabaka la chini kabisa (Ngaiza, 2002).

Mawazo haya yanaungwa mkono na mtazamo wa Marx (1859) kuwa mali na fedha ni vitu ambavyo vinaweza kusababisha haki za watu kupotea. Kitendo cha familia ya Cheja kutaka kulipwa fidia kwa kitendo cha binti yao kubakwa ni kumnyima haki yake ambayo angeipata katika mahakama. Hata hivyo, wakati mwingi haki inaweza isipatikane mahakamani kutokana na kuwepo kwa rushwa katika jamii. Yote hii inasababishwa na tamaa ya fedha na mali iliyoasisiwa na mfumo wa kibepari katika jamii.

#### 4.3.3.1 Mwanamke ni Mshauri Mzuri katika Jamii

Mwandishi Penina Mlama anamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye uwezo wa kutoa ushauri mzuri katika jamii ya Watanzania. Ni ukweli usiokuwa na shaka ndani

yake ambapo tunaona namna mwanamke katika jamii alivyomsitari wa mbele katika kutoa shauri nzuri lakini mara chache sana shauri hizo hufuatwa na wanajamii hasa wananume. Hii inatokana na mfumo dume uliopo katika jamii unaomuona mwanamke kuwa ni kiumbe asiye na uwezo wa kutoa ushauri wenye manufaa kwa jamii na ni mwanaume pekee ndiye mwenye uwezo huo. Penina Mlama anasema:

> BI. CHOWE: Niacheni jamani. (Anarudi kwa Cheja.) Uuuuuuui! Mwenzenu nimemkosea nini Mungu mieeeeeeeeeee!
>
> BW. CHOWE: Kelele wewe! Usiniitie kijiji kizima kwa yowe zako. Niache hasira zangu ziishie kwa Sembuli. Sembuli! Sembuli! Nitakwenda nikamkute huko aliko. Nitaua mtu mimi jamani.
>
> MWANAMKE II: Hapana, baba, hapana. Usiyachukulie mambo kwa ghadhabu. Usijihangaishe kumfuata unaweza usimuone. Na nani ajuae, kwenye jiji kubwa kama Dalisalama lolote linaweza likutokee. Baraza letu la wazee mbona lipo na wewe ukiwa mmoja wao. Yafanyeni mashtaka haya kimila tu (uk. 14-15).

Dondoo hili linaonesha namna wazazi wa Cheja walivyopatwa na hasira baada ya kupata taarifa kuwa Sembuli ndiye aliyemtia mtoto wao ujauzito. Mama yake Cheja alilia huku akipiga yowe jambo lililomkera mumewe na kumuonya kuwa ni vema aache yowe hizo kwani zitajaza umati wa watu nyumbani kwao. Badala yake yeye baba yake Cheja atafunga safari kwenda kumshughulikia Sembuli huko huko katika jiji la Dar es Salaam ili amazilize hasira zake. Hata hivyo, mwanamke mmoja ambaye ni mhusika katika tamthiliya ya *Hatia* anatoa ushauri kuwa si vyema kwa Bw. Chowe kwenda Dar Salaam bali Sembuli aitwe katika kikao cha Baraza la Wazee na suala la kubaka na kumtia mimba Cheja lijadiliwe na kupatiwa ufumbuzi.

Mwanamke huyo alikuwa ni mtu mwenye hekima na busara aliyefahamu kuwa madai ya kuwa Sembuli amehusika katika kumtia mimba Cheja ni tuhuma tu ambazo zilikuwa bado kuthibitishwa. Iwapo baba yake Cheja atakwenda Dar Salaam na kupambana na Sembuli kwa namna yoyote ile halafu baade ikaja kufahamika kuwa mambo hayakuwa hivyo ingekuwa ni jambo la aibu sana kwa Bw. Chowe mbele ya Sembuli na jamii nzima.

Ushauri wa mwanamke huyo ulikuwa na maana kubwa na ulisikilizwa na shauri lililetwa mbele ya baraza la wazee. Wanawake kama hawa wapo katika jamii na wanatakiwa wapatiwe fursa na kusikilizwa pale wanapotoa ushauri juu ya jambo kutokana na ukweli kuwa shauri za wanawake mara nyingi huwa zina tija ndani yake. Hii haina maana kuwa wanaume hawawezi kutoa shauri zenye tija la hasha, bali kutokana na mfumo dume uliopo shauri za wanawake hudharauliwa na za wanaume huonekana kuwa ndio bora (Koda, 2000).

### 4.3.4 Umasikini katika Jamii

Umasikini ni dhamira inayosawiriwa katika kazi za fasihi tangu ulimwengu wa fasihi simulizi mpaka leo. Hii ni kutokana na ukweli kuwa umasikini ni tatizo kubwa linaloikabili jamii tangu enzi na enzi na kuondoka kwake ni kazi ngumu (Ramadhani, 2005). Umasikini ni dhamira pana iliyogawanyika katika aina mbalimbali kama vile, umasikini wa kipato, umasikini wa ufahamu na uchambuzi wa mambo (umasikini wa fikra), umasikini wa kupata huduma mbalimbali za kijamii kama afya, elimu, maji, usafiri, umeme na pembejeo za kilimo (Omary, 2011). Hali ya umasikini wa aina hii huwafanya wanajamii kuishi maisha ya taabu na kero nyingi ambazo huwafanya kuyaona maisha kuwa ni magumu sana.

Mwandishi Penina Mlama anaisawiri dhamira ya umasikini katika tamthiliya ya Hatia kwa kuthibitisha kuwa umasikini bado ni tatizo kubwa linaloikabili jamii ya Watanzania licha ya kuwepo mikakati mbalimbali ya kupambana na umasikini na kukuza uchumi nchini Tanzania. Mwandisi anasema:

> BI. CHOWE: Jamani tayari yameiva. Tupepete sasa.
>
> MWANAMKE I:Huyu naye mvivu. Kila siku hupepeta mahindi kabla hayajawa tayari.
>
> MWANAMKE II: Ndiyo kazi yake huyo.
>
> BI. CHOWE: Ee jamani shauri ya uzee. Hivyo na mwanangu Cheja mnamuona amekuwa mama mzima bado mnategemea nina nguvu za kutwanga tu. Kwanza hii yote shauri ya umasikini tu. Mwanangu asingekwenda kufanya kazi Dalisalama saa hizi mimi kazi yangu tu ni kufanyiwa kila kazi.
>
> MWANAMKE I: (Anaanza kupepeta) Thubutu! Angekuwa ameshaolewa anawafanyia kazi wakwe zake na wewe ungebaki hapa hapa (uk.10).

Katika dondoo hili kunasawiriwa dhamira ya umasikini waliokuwa nao Bi. Chowe na familia yake kuwa ndio uliomfanya mtoto wao Cheja kukimbilia mjini kwa lengo la kutafuta maisha mazuri. Kutokana na hali hiyo mama yake Cheja analazimika kutwanga mahindi ambayo hata hivyo yanamshinda kutokana na kukosa nguvu kazi ambayo ilistahili kufanywa na wasichana kama akina Cheja. Umasikini ni miongoni mwa sababu kubwa zinazowafanya watoto wa kike kuondoka nyumbani kwao kwenda mijini kutafuta maisha. Watoto hao mara nyingi huwa ni wale ambao bado hawajapata akili na uwezo wa kujitambua jambo ambalo huwafanya kuishi maisha ya kudanganywa na kupatiwa ujauzito wangali bado watoto. Kutokana na hali hiyo

wengi wao huzaa watoto ambao hukosa malezi ya baba na mama na watoto wao kuishia kuwa watoto wa mitaani (Mwaipopo, 1990).

Dondoo hili pia linaonesha kuwa umasikini ni moja kati ya mambo yanayowasabisha watu wazima ambao wamefikisha umri wa kupumzika kufanya kazi kuendelea kufanya kazi licha ya kukosa nguvu za kufanya hivyo (Omary, 2011). Jambo hili lina uhalisia usiopingika katika maisha ya jamii kwani katika sekta mbalimbali baadhi ya watumishi ambao wamefikisha umri wa kustaafu bado wanaendelea kufanya kazi. Katika hali ya kawaida wastaafu wote wanatakiwa kupumzika nyumbani na kujihusisha na shughuli zao ndogondogo za kijasiriamali na kilimo na sio kuendelea na kazi za utumishi katika sekta za umma. Hali hii huwanyima fursa ya ajira vijana ambao wamemaliza masomo yao na kukosa ajira kwa sababu wastaafu bado wanaendelea kushika ajira hizo. Hii yote inasababishwa na umasikini uliopo katika jamii na hata katika serikali ambapo hushindwa kuwalipa watumishi wake mishahara na marupurupu mazuri ili waweze kufanya uwekezaji utakaowasaidia mara baada ya kustaafu. Kutokana na ukweli huu inakuwa ni jambo gumu kwa baadhi ya wastaafu kuweza kuishi maisha mazuri mara baada ya kustaafu na kulazimika kuomba kuendelea kufanya kazi hata baada ya kustaafu.

Katika dondoo lililopo hapo juu kunaoneshwa pia umasikini umeitawala jamii hasa jamii za vijijini kiasi cha kukosa mashine ya kusagia nafaka na kulazimika kutwanga mahindi kama njia ya kupata unga wa kupikia ugali na uji. Hii inatokana na vijiji vingi kukosa umeme na hivyo kuwa vigumu kuwepo na mshine za kusaga za bei nafuu. Mashine zilizopo katika baadhi ya vijiji ni zile ambazo zinatumia mafuta ya dizeli na hivyo gharama ya kusaga mahindi na aina nyingine za nafaka ni kubwa

isiyowezekana kulipwa na wananchi wa kipato cha chini kama wale wa vijijini. Jambo hili linaweza likazua mjadala kwamba, hivi kweli inawezekana mtu wa kijijini akakosa shilling 500 kwa ajili ya kusaga mahindi mashineni? Jibu la swali hili linaweza kuelezwa kwa urahisi tu kuwa haiwezekani mtu akakosa shilling 500 ya kusaga unga. Ukweli wa mambo ni kuwa upo uwezekano mkubwa wa mwananchi wa kijijini kukosa shilling 500 kwa ajili ya kusaga nusu debe la mahindi kwa sababu kijijini hakuna mzungunguko mkubwa wa fedha kama ilivyo katika maeneo ya mijini.

Mehring (1962) anaeleza kuwa maeneo ya vijijini husahauliwa katika maendeleo ya taifa kwa sababu hakuna viongozi wanaoishi katika maeneo ya vijijini. Binadamu ni mtu mbinafsi kwa asili na hivyo viongozi ambao ndio wanaopanga miradi mbalimbali ya maendeleo hupendelea maeneo wanayokaa na kusahau maeneo ya vijijini (Bell, 1977). Hali hii husababisha maeneo ya vijijini kuwa nyuma kimaendeleo na kuwafanya watu wake kuwa masikini wa mwisho kabisa katika jamii na katika nchi yao. Suluhisho la hali hii ni kuhakisha kuwa nyanja za elimu, afya, maji, umeme, barabara na makazi bora zinapewa vipaumbele katika bajeti ya fedha ya serikali ya kila mwaka. Sambamba na hilo pia pembejeo za kilimo zinapaswa kupatikana kwa wingi katika maeneo ya vijijini tena kwa gharama nafuu zaidi. Hii itasaidia kuendeleza kilimo ambacho ndicho kinachotoa ajira nyingi kwa Watanzania mpaka hivi sasa.

#### 4.3.5 Matabaka katika Jamii

Dhana ya matabaka katika jamii hutumiwa kurejelea uwepo wa makundi mawili katika jamii kundi moja likiwa ni la walionacho na kundi la pili likiwa ni la

wasionacho. Kuwepo kwa matabaka katika jamii ndio msingi wa jamii hiyo kuweza kupata maendeleo yake hasa pale tabaka tawaliwa linapofanya jitihada ya kulipindua tabaka tawaliwa ili kupata afuweni ya maisha. Harakati hizo husaidia kutokea kwa mabadiliko katika jamii ambayo hupelekea maendeleo kutokea pale wananchi wa kipato cha chini wanapopata afuweni ya maisha. Matabaka ya masikini na matajiri yamekuwepo katika jamii katika vipindi vyote vya maisha isipokuwa katika kipindi cha Ujima ambapo watu wote waliishi na kumiliki mali kwa pamoja. Katika jamii ya leo hali ya matabaka imeongezeka kwa kasi sana kiasi kwamba tabaka la walionacho na wasionacho ni kubwa lisiloelezeka kwa urahisi. Linebaugh (1976) anaeleza kuwa chanzo kikuu cha kuongezeka kwa matabaka katika jamii ni watu wachache kumiliki rasilimali za uzalishaji mali kama ardhi, mitaji, madini na nguvu kazi ya taifa.

Mwandishi Penina Mlama ameona namna matabaka katika jamii unavyokua kwa kasi kubwa na ndipo alipoamua kusawiri hali hiyo katika tamthiliya ya *Hatia*. Katika tamthiliya hiyo anaonesha kuwa katika jamii ya Watanzania kuna matabaka ya watu matajiri sana na wengine masikini sana. Haya yanabainika pale anaposema:

> MKAMI: ndio, kwanza huyu dada yangu angeolewa vizuri angepata zaidi ya hizo. Sasa yeye kajitia kumharibu basi lazima alipe. Kwanza yeye tajiri. Mtu ana hata gari.
>
> MZEE CHIMAISI: Hata! Hapana. Mambo hayaendi namna hiyo. Kwanza lazima tupate mzee mmoja upande wa Sembuli kusimamia madai haya. Mmoja wenu nyie; (kwa mzee 4na 5) mmoja wenu nyie msitazamane tu na mtoto ni wenu wenyewe.
>
> MZEE 5: Tena basi. Kwani mmesahau wakati wa harusi yake huyohuyo Sembuli tulivyofanya.
>
> MZEE 6: Eti kweli. Si tulipigania mpaka tukafikia malipo nusu ya yale yaliyotajwa kwanza. Lakini leo shauri lake. Atalipa hata kama ikimlazimu kuuza gari lake wala sisi hatutamtetea.

Mawazo yanayopatikana katika dondo hili yanaonesha kuwa katika jamii kuna matabaka ya walionacho na wasionacho. Mkami anaonekana kutaka malipo makubwa ya fidia ya dada yake kubakwa na Sembuli na kuonesha bayana kuwa Sembuli anao uwezo wa kulipa fedha hizo na kama akishindwa basi atalazimika kuuza gari lake. Mawazo haya ya Mkami yanaungwa mkono na Mzee 6 ambaye naye anarudia maneno yale yale yaliyosemwa na Sembuli. Hii inaonesha kuwa Sembuli ni mtu aliye tabaka la juu na akina Mkami pamoja na watu wengine wa kijijini ni watu waliopo katika tabaka la chini. Kitendo cha mtu kumiliki gari wakati watu wa kijijini hawana hata fedha ya kusaga mahindi kinaonesha utabaka uliokithiri katika jamii ya Watanzania.

Hii ni hali halisia kabisa katika maendeleo ya jamii zetu ambapo katika kipindi hiki watu wa mijini hasa viongozi wamekuwa wakijilimbikizia mali kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa na ufisadi jambo linalowafanya wao kuwa matajiri wakubwa na masikini kuendelea kuwa masikini zaidi. Marx (1847) anaielezea hali hii kuwa inatokana na ubinafsi alionao mwanadamu katika nafsi yake ambao humfanya kujijali yeye binafsi pamoja na familia yake huku akiwasahau kabisa wanadamu wengine. Jambo la kushangaza ni kuwa, malimbikizo ya mali yanayofanywa na kiongozi huyu yanatokana na kodi ya wananchi hao hao masikini aliowajali na kujijali yeye binafsi. Huu bila shaka ni udhalimu mkubwa ambao unaongeza kasi ya kuwepo kwa matabaka katika jamii ya Watanzania.

Katika dondoo lililopo hapo juu pia imeoneshwa kuwa wananchi wa kawaida wanachukia kuona matajiri wakijilimbikizia mali na wao wakiendelea kuwa masikini wa kutupa. Kauli kama, “hata ikiwezekane auze gari lake apate fedha za kulipa

faini," ni kauli yenye kuonesha wananchi kutoridhishwa na mwenendo mzima wa baadhi ya viongozi kujilimbikizia mali na kuwaacha wananchi wa kawaida wakiteseka na hali duni ya maisha. Hivyo, huu ni wakati wa viongozi kutambua kuwa wananchi wa leo wameshapata ufahamu wa mambo kwa kiasi cha kutosha na hakuna mtu anayeweza tena kuwadanganya kwani wanafahamu uhalisia wa mambo vile ulivyo na wapo tayari kwa mabadiliko.

## 4.4 Muhutasari

Katika sehemu hii tumewasilisha na kuchambua data za utafiti zilizosaidia kukamilika kwa malengo mawili mahususi ya utafiti huu ambapo lengo mahususi la kwanza na la pili yameunganishwa pamoja kutokana na kukaribiana kimantiki. Dhamira za kijamii zilizowasilishwa katika sehemu hii ni uongo katika jamii, penye ukweli uongo hujitenga, nafasi ya mwanamke katika jamii, umasikini katika jamii na matabaka katika jamii ya Watanzania. Katika kila dhamira tumeonesha ni kwa vipi dhamira hiyo imesheheni uhalisia katika jamii ya leo ya Watanzania. Katika sehemu inayofuata tumewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti zinazohusiana na lengo mahususi la tatu la utafiti huu juu ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama.

## 4.5 Mbinu za Kisanaa katika Tamthiliya ya *Hatia*

Lengo mahususi la tatu la utafiti lilihusu matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Tunapozungumza juu ya mbinu za kisanaa tunamaanisha ule ufundi wa kisanaa uliotumiwa na mwandishi katika kuandika au kuwasilisha kazi yake kwa hadhira iliyokusudiwa. Matumizi ya mbinu za kisanaa katika kazi za fasihi ni taaluma pana sana ambayo hatuwezi kuelezea na

kuwasilisha katika kazi hii tukamaliza. Hata hivyo, katika kutimiza lengo mahususi la tatu la utafiti huu tumewasilisha, kuchambua na kujadili mbinu tano za kisanaa kama zilivyotumiwa na Penina Mlama katika *Hatia*.

### 4.5.1 Matumizi ya Nyimbo katika Tamthiliya ya *Hatia*

Nyimbo ni kipera cha utanzu wa ushairi wa fasihi simulizi kilichotumika katika karne nyingi kwa dhima mbalimbali katika jamii si ya Waswahili tu bali jamii zote Afrika na ulimwenguni kote. Hii ni sawa na kusema kuwa, nyimbo zina historia ndefu sana inayofungamana na historia ya mwanadamu kuanza kuwasiliana na wanadamu wenzake kwa kutumia lugha (Khatibu, 2014). Jamii za Kiafrika zilibuni nyimbo mbalimbali ambazo walizitumia katika kuchapusha kazi kama za kilimo, ufugaji, ufumaji, ususi, uchoraji na uchongaji kwa lengo la kuleta tija na ufanisi katika shughuli hizo za uzalishaji mali (Mulokozi, 1996). Wanadamu duniani kote walipokuwa katika kipindi cha Ujima ambapo hakukuwa na maendeleo ya teknolojia ya kuwawezesha kufanya kazi zao za uzalishaji kwa haraka walilazimika kubuni nyimbo ambazo zilifungamana na ngoma ili kuwaburudisha wakati wanafanyakazi. Lengo hasa lilikuwa ni kuwafanya wasichoke katika kufanyakazi na kujikuta wameweza kufanya kazi kubwa kwa siku moja bila wao wenyewe kujitambua (Mulokozi, ametajwa).

Matumizi ya utanzu wa nyimbo hayakuishia katika kuchapusha na kuhamasisha wanajamii kufanya kazi bila ya kuchoka peke yake bali yalikwenda mbali zaidi na kuhusika katika shughuli mbalimbali za kijamii. Nyimbo kama vile za harusi na ndoa, misiba, kuapishwa na kutawazwa kwa viongozi, kampeni za kisiasa, nyimbo za dini na nyimbo za jando na unyago (Wamitila, 2003). Hii inaonesha kuwa karibu

kila jambo katika jamii linafungamana na matumizi ya nyimbo maalumu wakati linatendeka. Leo hii katika jamii ya Watanzania kuna uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika tarehe 25 mwezi wa 10 mwaka 2015 na kampeni za wagombea kuomba kura za wananchi zinaendelea kila kona ya nchi. Katika kampeni hizo kila mgombea amekusanya wanamuziki pamoja na bendi mbalimbali za kutumbuiza wakati mgombea akiomba kura.

Kutokana na umuhimu na nafasi ya nyimbo katika jamii inakuwa si jambo la kawaida kwa mtunzi wa kazi fulani ya fasihi kama vile tamthiliya, hadithi na riwaya kukosa matumizi ya nyimbo ndani ya kazi yake hiyo. Wataalamu wa fasihi huiita hali hii kuwa ni mwingiliano wa tanzu ambapo wimbo au nyimbo ni utanzu mwingine na tamthiliya ni utanzu mwingine lakini unakuta kimoja kipo ndani ya kingine. Mwandishi Penina Mlama ni mmojawapo kati ya watunzi wa kazi za fasihi ambaye ametumia nyimbo katika tamthiliya ya *Hatia*. Kwa mfano:

> Sikilizeni! Sikilizeni!
> Hapa si kijijini,
> Ohoo Ohoo Ohoo Ohoooo!
> Sikilizeni! Sikilizeni!
> Hapa ni mji mkubwa
> Ohoo Ohooo Ohoo Ohooo! (uk.07).

Matumizi ya wimbo huu yanajitokeza mwanzoni kabisa mwa onesho la kwanza la tamthiliya ya *Hatia* ukiwa na dhima kuu ya kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Mutembei (2012) anaeleza kuwa matumizi haya ya wimbo mwanzoni wa tamthiliya hii yametumiwa kama mbinu ya kisanaa ya kikorasi. Hii ina maana kuwa matukio mengi yanayojitokeza ndani ya tamthiliya ya *Hatia* tayari hadhari yake imekwishatolewa katika wimbo huu. Mathalani, katika tamthiliya ya *Hatia* tunamuona mhusika Cheja akidanganywa na Juma na kupatiwa ujauzito na baada ya

hapo anasingizia kuwa aliyempa ujauzito ni Sembuli. Hii ilitokea baada ya Juma kukataa kuwa ujauzito alionao Cheja si wake na kwamba Cheja akitaja kuwa Juma ndiye alimpa ujauzito atakiona cha mtemakuni.

Kwa jumla, matumizi ya wimbo huo hapo juu yanaonesha kuwa mjini ni mahali ambapo kuna vishawishi vya aina mbalimbali ambavyo vinaweza kumfanya mtu akajikuta amefanya mambo ambayo hajakusudia wala kufikiri kwamba siku moja atafanya. Ndio maana katika wimbo huo anasema, “Hapa ni mjini sio kijijini,” akiwa na maana kuwa maisha ya mjini hasa Dar es Salaam ni tofauti kabisa na maisha ya kijijini alikotoka Cheja. Hivyo, mgeni kutoka kijijini anapoingia mjini anatakiwa kuwa makini kwa kuchukua hadhari kwa kila jambo analolifanya.

Matumizi ya wimbo huo katika onesho la kwanza la tamthiliya ya *Hatia* linatuonesha kuwa mwandishi hakutumia hivi hivi tu bali kwa lengo maalumu ambalo ni kumtaka msomaji kuwa mbunifu na mzingativu kwa kile atakachokisoma ndani ya tamthiliya husika. Karibu kila tukio lililoelezwa katika tamthiliya ya *Hatia* linarejelea au kufumbatwa katika wimbo huo kikorasi kama anavyoita Mutembei (2012).

Msomaji makini wa tamthiliya ya *Hatia* atajiuliza maswali swali hivi kwa ni kwa nini mwandishi ametumia wimbo mwanzoni tu mwa onesho la kwanza la tamthiliya yake? Bila shaka kuna kitu ambacho anataka sisi kama wasomaji tukipate. Baada ya kujiuliza swali hili na kuendelea kusoma tamthiliya hii ndipo sasa anapobaini kuwa karibu kila jambo linalosemwa katika tamthiliya hii linafungamana na maneno ya wimbo huo.

Wimbo huo hapo juu umeundwa na kueleza mambo kwa kuzingatia matabaka ya watu wa mjini na watu wa kijijini. Bell (1977) anaeleza kuwa maisha ya mijini mara nyingi ni ya kibepari ambapo kila mtu anajitegemea katika maisha yake yaani yeye binafsi pamoja na familia yake. Si jambo la kawaida kwa mtu wa kijijini kwenda kuomba unga, mboga, chumvi au sukari kwa jirani yake kwa sababu vitu hivyo hununuliwa kwa fedha katika maduka na masoko. Lakini maisha ya kijijini ni tofauti ambapo watu huishi kwa pamoja na kusaidiana kwa kila jambo. Ikiwa jirani ameishiwa unga, chumvi, mboga au sukari anaweza kwenda kwa jirani yake na akapewa bila tatizo na kuendelea na maisha yake. Hivyo, Cheja anavyoambiwa kuwa maisha ya mjini si sawa na ya mjini hiyo ndiyo dhana yenyewe ambayo wasomaji wa Hatia wanapaswa kuipata.

### 4.5.2 Matumizi ya Takriri

Takriri ni mbinu ya kisanaa inayotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi kwa lengo la kusisitiza au kuonesha uzito wa dhamira fulani kwa jamii (Njogu na Chimerah, 1999). Senkoro (2006) anaeleza kuwa wakati mwingine mbinu ya takriri hujulikana kama mbinu ya marudiorudio ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza akarudia silabi, neno, sentensi au aya nzima kwa makusudio maalumu na hasa kusisitiza jambo ambalo anataka hadhira yake ilipate.

Anaendelea kueleza kuwa mbinu hii kwa asili ni mbinu ya fasihi simulizi lakini leo inatumika pia katika kazi za fasihi andishi za riwaya, ushairi, tamthiliya na hadithi fupi. Ukitazama tanzu na vipera mbalimbali vya fasihi simulizi utaona matumizi ya takriri yakijitokeza sana katika semi, hadithi, ushairi na sanaa za maonesho. Kwa mfano katika methali kuna methali isemayo, “haba na haba hujaza kibaba,” ambapo

neno “haba” limerudiwa mara mbili kutoa msisitizo kuwa kuweka akiba kidogokidogo ni jambo muhimu sana kwani baada ya muda akiba hiyo huwa nyingi kuisaidia mtu kufanya mambo ya msingi katika maisha.

Mwandishi Penina Mlama ametumia mbinu ya takriri katika tamthiliya yake kwa kiasi kikubwa akiwa na lengo la kusisitiza dhamira mbalimbali ambazo anataka hadhira yake izielewe. Katika kutumia mbinu hii mwandishi ametumia takriri silabi kuonesha uzito wa mambo fulani. Kwa mfano:

> CHEJA: Bwana Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi ni mjamzito. (Wote wanapigwa bumbuazi).
>
> BW. CHOWE: Eti nini? (Cheja anaanza kulia).
>
> BI. CHOWE: Uuuuuuui, Uuuuuuuuuui Mungu wangu! (kwa wanawake wenzie) Jamani nielezeni labda sikusikia vizuri. Uuuuuuuuuuuuui! (Anamkimbilia Cheja). Cheja mwanangu Uuuuuuuuuuui!
>
> BW. CHOWE: (kwa Bi. Chowe) Aaa! Acha kelele wewe. Sema vizuri Cheja sema acha kulia! Ati kweli au unatania?
>
> CHEJA: Kweli baba.
>
> BI. CHOWE: Uuuuuuuuui! Uuuuuuuuuui! (Anakwenda kwa wanawake wenziwe). Uuuuuuui!

Katika dondoo hili mwandishi ametumia takriri silabi, “Uuuuuuuuui,” inayoonesha kilio cha Bi. Chowe mara baada ya kusikia maneno kutoka kwa mtoto wake akidai kuwa amebakwa na Sembuli. Matumizi haya ya takriri yanaonesha uchungu alioupata mama yake Cheja baada ya kusikia kitendo kiovu alichofanyiwa mtoto wake akiwa ugenini huko Dar es Salaam. Hii inaonesha kuwa mama ni mtu ambaye huwa anapata uchungu zaidi kuliko baba anaposikia jambo baya limefanywa au

limepata mtoto wake. Wataalamu wa masuala ya jinsia wanaeleza kuwa hali hii huwapata akina mama huwa wanaumwa sana na tumbo wanaposikia kuwa mtoto waliyemzaa amepata tatizo fulani. Hii inatokana na kubeba ujauzito miezi tisa na baadae kumlea mtoto mpaka anafikisha umri wa kujitegemea mwenyewe (Koda, 2000). Hii inamfanya mama kuwa ni mtu wa karibu sana na mtoto kuliko baba na anaposikia mtoto amepata tatizo mama hujisikia vibaya sana.

Matumizi mengine ya takriri yanajitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* pale Cheja anaposhangaa maneno ya Juma kuwa asitajwe popote kuwa yeye ndiye aliyempa Cheja ujauzito. Mwandishi anasema:

> CHEJA: (kwa hamaki) Juma! Huwezi kwenda namna hii hata kidogo. Huwezi kunikana na hali ulisema unanipenda. Nilikueleza siku ile hatari yake hukutaka kunisikia. Ukajisingizia mapenzi. Sasa leo unataka kunikana hivi. Hata kidogo!
>
> JUMA: Hata kikubwa. Usinishikilie hivyo. Tena nakueleza wazi usije ukalogwa kumwambia mtu kuwa mzigo huo ni wangu. Walahi utajuta.
>
> CHEJA: Utafanya nini?
>
> JUMA: (Anacheka.) Eti "utanifanya nini" kwanza utaniona wapi? Kwanza nani shahidi?
>
> CHEJA: (kwa uchungu.) Yaani kweli, Juma imekuwa si kitu kwako litakalonipata baadae. Hunifikirii nitamfanyaje mtoto. (Anashindwa kusema kwa muda.) Kumbe yote yalikuwa ulaghai mtupu. Siamini! Siamini!
>
> JUMA: Amini! Amini tu! Wewe sikiliza. Jiendee zako kwa wazazi wako ukajitunze kama unaogopa kuendelea kukaa kwa mwajiri wako. Nenda tu (uk.09).

Matumizi ya takriri katika dondoo hili yanajitokeza pale Cheja anaposema, "siamini, siamini," kuwa kweli Juma amekana kuwa mimba aliyonayo Cheja si yake na hali ya

kuwa alimwahidi kuwa anampenda sana. Takriri hii ni ya mshangao na msisitizo kuwa hivi ni kweli Juma aliyekuwa akizungumza maneno mazuri ya kimapenzi kuwa anampenda sana Cheja lakini alipopata alichokuwa anakitaka anakataa ujauzito wa Cheja. Juma naye anatumia takriri, “amini, amini tu! Kutoa msisitizo kuwa anachokisema kuwa haitambui mimba ya Cheja ni hakika kabisa.

Marx (1859) anaeleza kuwa masuala kama haya hutokea katika jamii za kibepari ambapo watoto wadogo wanakuwa na uhuru mkubwa wa kufanya mambo bila ya muongozo wa wazazi wao. Mfumo wa maisha ya kijamaa unaopendekezwa na Karl Marx ndiyo ulio bora katika kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa katika malezi mema ambayo hayatawafanya kujihusisha na ngono za utotoni na kupata mimba wakiwa watoto wadogo. Maelezo haya ya Marx ni ya kweli kwani katika jamii ya leo watoto wadogo wamekuwa na uhuru mkubwa wa kufanya mambo makubwa kuliko umri wao na kuingia katika matatizo mbalimbali ikiwemo kupata UKIMWI na mimba za utotoni. Wazazi wanapaswa kuwa makini sana katika kuhakikisha kuwa watoto wao ambao bado hawajawa na umri wa kujitegemea na kujitambua hawaondoki nyumbani na kwenda mijini kutafuta kazi. Hii itasaidia sana kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa na maadili mema na hasa kwa watoto wa kike wanaepuka mimba za utotoni.

### 4.5.3 Matumizi ya Tafsida

Tafsida ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kwa lengo la kuficha au kupunguza ukali wa maneno ambayo kwa kawaida haipendezi kuyajata waziwazi katika hadhara ya watu (Wamitila, 2003). Kila jamii ya watu duniani ina utamaduni wake ambapo kunakuwa na maneno ambayo hayatamkwi

hadharani kwa lengo la kuimarisha maadili mema katika jamii hiyo. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Watanzania masuala yanayohusu mapenzi na ngono hayapaswi kutamkwa bayana katika hadhara. Lugha ya aina hiyo hutambuliwa kuwa ni lugha ya ndani na mahali pake ni huko ndani na si nje. Licha ya maneno na lugha inayohusu masuala ya mapenzi na ngono yapo mambo mengine pia ambayo hayawezi kutajwa mbele za watu kutokana na miiko ya jamii.

Mwandishi Penina Mlama ni miongoni mwa watunzi wa kazi za fasihi anayeheshimu sana mila, desturi, tamaduni na miiko ya jamii na kwa hivyo anatumia tafsida katika kazi zake. Tamthiliya ya *Hatia* ni moja kati ya kazi zake iliyosheheni matumizi ya tafsida. Katika tamthiliya hii mwandishi ametumia tafsida pale aliposema:

> CHEJA: Sikuweza kuvumilia kukaa tena nyumbani kwao. (Anatazama chini.) Hapana sikuweza.
>
> BW. CHOWE: Kwa nini?
>
> CHEJA: (Kwa kusita hali akiwa bado anatazama chini.) Bwana Se … Bwana Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi ni mjamzito.

Dondoo lililopo hapo juu lina matumizi ya tafsida pale mwandishi anaposema, “bwana Sembuli alinikosea kwa nguvu na sasa mimi ni mjamzito.” Katika hali ya kawaida alipaswa kusema kuwa “Sembuli alimbaka na hivi sasa yeye (Cheja) ana mimba.” Kauli hi haipendezi sana kusikika katika masikio ya mwanadamu ukilinganisha na ile ya kwanza. Huu ndio ustaraabu na utu wa mwanadamu. Kama tulivyoeleza mahali fulani huko nyuma kuwa masuala yanayohusu ngono huwa hayatajwi hadharani na tena inapokuwa mbele ya wazazi huwa ndio mwiko mkubwa zaidi. Hivyo, Cheja alipotamka kuwa “Sembuli alikosea,” tayari wazazi wake

walikwishaelewa kuwa alikuwa anazungumzia kitu gani na hivyo hawakuwa na haja ya kutaka ufafanuzi zaidi kutoka kwa mtoto wao.

Vilevile, Katika dondoo hilo tunaoneshwa kuwa haipendezi kutamka waziwazi kuwa mwanamke ana mimba bali mwanamke ana ujauzito. Inafahamika kuwa neno mimba linafaa zaidi kurejelea wanyama kuliko mwanadamu na hivyo kila mwanajamii hutumia neno “ujauzito” kumrejelea mwanamke mwenye mimba. Huu ndio uhalisia wa mambo kama ulivyo katika jamii ya maisha ya leo.

### 4.5.4 Matumizi ya Muundo katika Tamthiliya ya Hatia

Muundo ni moja kati ya vipengele muhimu vinavyounda fani ya kazi ya fasihi simulizi na andishi. Muundo ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi ya fasihi unaonesha namna kazi hiyo ilivyopangwa tangu mwanzo mpaka mwisho (Njogu na Chimerah, 1999). Kuna aina mbalimbali za muundo katika kazi ya fasihi kulingana na ujuzi na mapenzi ya mtunzi kuwa yeye anataka kutumia muundo gani ili kuwasilisha dhamira kwa wasomaji wake. Aina hizo za muundo ni muundo wa moja kwa moja, muundo rejeshi, muundo changamano na muundo tata.

Mwandishi Penina Mlama ametumia muundo wa moja kwa moja katika kuwasilisha matukio katika kazi yake. Muundo wa moja kwa moja katika tamthiliya ya *Hatia* umejengwa kutokana na maonyesho sita kwa kila onyesho kukamilisha onyesho lingine. Katika kuonesha kuwa mwandishi anatumia muundo wa moja kwa moja tazama maneno ya yanayotolewa na Mvuvi katika onyesho la Kwanza.

> Mvuvi: Kila siku samaki, samaki, samaki; lakini kwanza hebu niwapange kabisa. Hawa nitawauza shilingi mbili mbili, hawa shilingi shilingi na hawa thumuni, soko kuu Kariakoo. Sasa hebu nijumlishe zitatoka kiasi gani.

> (Anahesabu kimya kimya. Cheja anakuja kutoka upande alikotokea mvuvi na kushtuka). Eee! Mama wewe! Hatari kujiendea hovyo tu. Kama mambo yenyewe ndio kwenda tu bila kutazama walahi utajikuta uko dunia ya pili. Ohoo! Shauri yako Dalisalama hii. (Anachukua kapu lake.) (uk.07).

Maneno haya ya mvuvi yanaonesha kuwa Cheja anafahamishwa kuwa sasa ameingia katika jiji la Dar es Salaam na kwamba anatakiwa kuwa makini kwani jiji hilo ni tofauti kabisa na kule alikotoka. Maneno haya ya mvuvi yanasadifu mfuatano wa visa na matukio katika tamthiliya nzima ya *Hatia* kwani visa na mikasa inayomkumba mhusia Cheja inatokana na maneno haya ya Mvuvi kama yanavyosomeka katika dondoo hapo juu. Maneno hayo yamelazimisha muundo wa visa na matukio katika tamthiliya hii kuwa ni ya moja kwa moja ambapo kila onesho limejengwa kutokana na onesho lililotangulia. Hii ni mbinu ya kipekee sana kupatikana katika utunzi wa tamthiliya ambapo maneno ya kwanza ya mhusika wa kwanza katika tamthiliya yanakuwa ndio yenye kujenga muundo wa tamthiliya yote. Si kila mwandishi anaweza kuwa na ubunifu wa aina hii bali ni wachache tu akiwemo Penina Mlama.

Katika kuendelea kuonesha kuwa tamthiliya ya *Hatia* imejengwa kutokana na muundo wa moja kwa moja hata mwisho wa tamthiliya yenyewe inathibitisha. Mwandishi anasema:

> MZEE CHIMAISI: Ngoja! Ngoja! Ameshatueleza kuwa huyo kijana hampendi Cheja na yeye Cheja mwenyewe hataki hata kumuona. Sasa Cheja ameazimia kuwa atakwenda kuanza maisha mapya kabisa.
>
> BW. CHOWE: Wapi tena, Dalisalama, atakaa hapahapa.

MZEE CHIMAISI: Aaah! Bwana sikiliza nimalize kwanza. Cheja anasema atakwenda Majogo kwenye kijiji kipya akajitegemee.

Maneno haya yanaonesha kuwa Cheja ameamua kutorudi tena mjini Dar es Salaam na kwenda kuanza maisha mapya katika kijiji kipya cha Ujamaa na kujitegemea kilichoanzishwa na serikali. Hii ina maana kuwa mwanzoni mwa mchezo tunaoneshwa kuwa alikuwa mjini akiwa pale alipokuwa akionywa na mvuvi na sasa yupo kijijini baada ya kukutwa na masaibu ya mjini. Huu ni muundo wa moja kwa moja ambapo visa na matukio vimepangwa kwa kuanza na tukio la kwanza na kuishia na tukio lililostahili kuwa la mwisho.

## 4.6 Hitimisho

Katika sura hii kumefanywa uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti wetu. Dhamira za kijamii zilizowasilishwa ni pamoja na kusema uongo katika jamii, penye ukweli uongo hujitenga, nafasi ya mwanamke katika jamii, mwanamke ni mshauri mzuri katika jamii, umaskini katika jamii na matabaka katika jamii. Dhamira zote hizi zimeonekana kuwa zina uhalisia kwani zinasawiri maisha ya kila siku ya jamii ya Kitanzania. Katika sura hii pia kumebainishwa mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira mbalimbali za tamthiliya ya Hatia. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya nyimbo, takriri, tafsida na muundo wa moja kwa moja.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii kumetolewa muhtasari, hitimisho na mapendekezo kuhusu utafiti utakaofanywa hapo baadae na watafiti wengine. Itakumbukwa kuwa hii ndio sura ya mwisho ya utafiti huu ambapo tumedokeza matokeo ya utafiti pamoja na kutoa hitimisho la jumla la utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na jumla ya malengo mahususi matatu ya utafiti yaliyotafitiwa na kukamilishwa kwa namna iliyowezesha kutimizwa kwa lengo kuu la utafiti huu. Malengo hayo mahususi yalikuwa ni kuelezea dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama, kutathimini uhalisia wa dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* kwa jamii ya leo ya Tanzania na kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika katika kuwasilisha dhamira za kijamii katika tamthiliya ya *Hatia*.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza na la Pili la Utafiti

Malengo mahususi la kwanza na pili ya utafiti huu yaliunganishwa kwa pamoja katika uchambuzi wa data kutokana na ukaribu wake kimantiki. Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lililenga kuelezea dhamira za kijamii zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa tamthiliya ya *Hatia* ina utajiri mkubwa wa dhamira za kijamii kama vile, kusema uongo katika jamii, penye ukweli uongo hujitenga, nafasi ya mwanamke

katika jamii, mwanamke ni mshauri mzuri katika jamii, umasikini katika jamii na matabaka katika jamii. Dhamira hizi kwa pamoja zimeonekana kuwa zina uhalisia katika maisha ya Watanzania licha ya tamthiliya hii kuandikwa takribani miaka 40 iliyopita. Kuhusu kusema uongo, jamii nyingi za Tanzania zikiwemo zile za mijini na vijijini hujihusisha katika kusema uongo kutokana na sababu mbalimbali hususani za kujinufaisha wao wenyewe. Mathalani, mtu anaweza kusema uongo ili apate fedha, mapenzi na vitu vingine anavyoona ni vizuri na vina manufaa makubwa katika maisha yake. Lakini mara apatapo kile alichokuwa anakihitaji, hubadilika na kushindwa kutekeleza ahadi alizoziahidi. Mfano mzuri ni ahadi za Juma kwa Cheja ambazo ziliyeyuka mithili ya theluji mara tu Juma alipopewa penzi na kumtia Cheja ujauzito.

### 5.2.2 Matumizi ya Mbinu za Kisanaa katika Tamthiliya Teule

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu lililenga katika kuchambua matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya *Hatia* iliyoandikwa na Penina Mlama. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, miongoni mwa mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi katika kuibua dhamira mbalimbali ni nyimbo, takriri, tafsida na muundo wa moja kwa moja. Mbinu hizi za kisanaa zimetumiwa kwa ustadi wa hali ya juu katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa hadhira iliyokusudiwa. Kwa mfano, matumizi ya wimbo mwanzoni tu mwa onesho la kwanza la tamthiliya ya *Hatia* limesaidia sana katika kutufahamisha hatima ya muhusika Cheja kutokana na kila jambo alilokuwa akilifanya au kumkuta lilihusiana moja kwa moja na maneno ya wimbo huo. Huu ni ufundi wa hali ya juu kabisa uliooneshwa na mtunzi wa tamthiliya hiyo ya *Hatia*.

## 5.3 Hitimisho

Kwa jumla tunaweza kuhitimisha kwa kueleza kuwa, tamthiliya ya Hatia ni moja kati ya tamthiliya nzuri ambayo bado inasawiri hali halisi ya maisha ya Watanzania licha ya kuwa imeandikwa miaka zaidi ya 40 iliyopita. Mafunzo na mafundisho yanayotolewa na mtunzi katika tamthiliya hii ni yale yanayomtaka kijana asiwe mwepesi wa kudhani kuwa maisha ya mjini ni mazuri na akitoka kijijini kwenda mjini atafanikiwa kwa urahisi zaidi kuliko kuishi kijijini. Mwandishi analiona suala hilo kama ni ndoto za alinacha kwa sababu halina ukweli wowote kwani maisha ya mjini ni magumu zaidi kuliko yale ya mjini. Ugumu wake unatokana na uhalisi wa maisha yenyewe ambapo kila kitu huuzwa na kununuliwa kwa fedha tofauti na maisha ya kijijini ambapo mtu anaweza kuomba kitu kwa jirani yake na akapata bila malipo yoyote. Kwa mijini hali haiko hivyo, kwani ni lazima mtu awe na fedha ndipo aweze kupata huduma fulani. Haya yote tunayapata kutokana na mikasa iliyompata mhusika Cheja katika tamthiliya ya *Hatia*.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu unapendekeza kuwa itakuwa vema kama utafiti kama huu utafanywa katika kuchunguza tamthiliya nyingine za Penina Mlama kwa lengo la kulinganisha na kulinganua dhamira za kijamii katika tamthiliya *Hatia* na hizo nyingine. Hii itasaidia kuupata muktadha mpana zaidi wa ujitokezaji wa dhamira za kijamii katika tamthiliya za mwandishi huyu maarufu wa sanaa za maonesho na tamthiliya za Kiswahili.

Pia, utafiti kuhusu matumizi ya mbinu za kisanaa katika tamthiliya ya Hatia unaweza ukafanywa ili kutoa picha kamili ya utaalamu wa Penina Mlama katika kuwasilisha

dhamira mbalimbali kwa wasomaji wake. Katika utafiti wetu tulichunguza matumizi ya mbinu za kisanaa kwa ufupi kwa kuwa halikuwa lengo kuu la utafiti huu hivyo, utafiti wa kina zaidi unaweza ukafanyika katika kipengele hiki.

# MAREJELEO

Aronson, J. (1992). "A Pragmtic View of Thematic Analysis in the Qualitative Report" Vol. 2 No. 1. Searched in. http:// www.nova.edu/scs/QR/Black Issues/QR21/aronson.html, on 23/05/2011, 11:00HRS.

Babbie, E., (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Bell, P. F. (1977), "Marxist Theory, Class Struggle and the Crisis of Capitalism" in Jesse Schwartz (ed.), *The Subtle Anatomy of Capitalism*. Santa Monica: Goodyear.

Benner, P. (1985), "Quality of Life: A phenomeno logical perspective on explanation, prediction and Understading in Nursing Science", *Advanees in Nursing Science*, 8(1), 1-14.

Beyanga, A. (2014), "Taswira ya Ng'ombe katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Washubi," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Creswell, J. W. (2009), *Research Design: Qualitative and Methods Approches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Daniel, Z. (2012), "Ubwege katika Tamthiliya ya *Amezidi*." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Engels, Frederick (1843), "Outline of a Critique of Political Economy" in *Marx & Engels Collected Works*, Vol, III 1843-44 New York: International Publishers.

Engels, F. (1892), "Introduction" to English edition of *Condition of the Working Class in England*. Stanford: Stanford University Press.

Good, G. V. (1966), *Essentials of Educational Research*. New York: Maridith Publications Co.

Hussein, E. (1983), "Hatua mbalimbali za kubuni na kutunga tamthiliya kufuatanana misingi ya Ki –Aristtotle." Katika, *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III FASIHI*. TUKI, Dar es Salaam.

Hussein, E. (1967), *Kinjeketile*, Oxford University Press Nairobi.

Hussein, E. (1971), *Mashetani*, Dar es Salaam, Oxford University Press.

Hussein, E. (1971). *Wakati Ukuta*. Nairobi: EAPH.

Hussein, E. (1976). *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1980). *Arusi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*, Oxford University Press.

Khalfan, M. Y. (2013), "Siasa katika Ushairi wa Saadana Kandoro: Mifano kutoka katika Mashairi yake." Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Kileo, S. (2013), "Dhamira katika Tamthliya ya *Kivuli Kinaishi*." Tasnifu ya kupata Shahada ya Awali, Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Koda, B. (2000) "The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District", Unpublished Ph.D Thesis, UDSM.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L.A. (2006), *Proposal and Thesis Writing*: Kenya, Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2008), *Reseach Methodogy: Methods and Techiniques*, New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Kumar, R. (1999), *Reserch Methodology Astep by guide for beginners*, New Delhi: SAGE Publication.

Ligembe, N. E. G (1995). *The Uses of Metaphor in Penina Muhando's Lina ubani. A stylistic analysis. Tasnifu* ya umahiri, (Haijachapishwa) University of Dar es Salaam.

Leininger, M. M. (1985), "Ethnography and Ethnonursing: Model and Modes of Qualitative Data Analysis". In. M.M. Leininger (Ed.). *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Pp (37-73). Oro lando FL: Grune& Stratton.

Linebaugh, P. (1976), "Karl Marx, the Theft of Wood, and Working-Class Composition: A Contribution to the Current Debate," *Crime and Social Justice*. Fall/Winter, pp. 5-16.

Marx, K. and Engels, F. (1848), "The Communist Manifesto" in *Marx & Engels Collected Works*, Vol. 6, 1845-1848. New York: International Publishers, 1976.

Marx, Karl. (1850), "Class Struggles in France," in *Marx & Engels Collected Works*, Vol. 10. New York: International Publishers.

Marx, Karl (1859) *A Contribution to the Critique of Political Economy*. New York: International Publishers 1970.

Massoud, S. M. A (2013), "Maudhui na Fani katika Tamthiliya za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za Mashetani na Kivuli Kinaishi," Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mehring, F. (1962), *Karl Marx, The Story of His Life*. Ann Arbor: University of Michigan Press.

Mlama, P. (1982), *Pambo*, Swala Publications: Dar es Salaam.

Mlama, P. (1983). "Utunzi wa Tamthiliya Katika Mazingira ya Tanzania." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI*. TUKI. Dar es Salaam.

Mlama, P. (1984). *Lina Ubani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mlama, P (1972) *Hatia.* East African Publishing House. Nairobi, Kenya.

Mohamed, S. A. (1990), *Kivuli Kinaishi*. Oxford University Press: Nairobi.

Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: EALB.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, TUKI: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, A. K. (2012), *Korasi katika Fasihi*, TATAKI: Dar es Salaam.

Mwaifuge, E. S. (2001), "Beliefs and Human Behaviour in the Theatre of Ebrahim Hussein," Unpublished M.A Thesis, University of Dar es Salaam.

Mwaipopo, R. N. G. (1990) "The Impact of Commodity Relations on the Role and Status of Women in Peasant Households: A Case Study of Rungwe District", M.A Thesis, University of Dar es Salaam.

Mwita, M. B. (2009), "Uhakiki wa Mtindo na Maudhui katika Baadhi ya Tamthiliya za Penina Muhando (Mlama)," Katika *Mulika* Na 28, Dar es Salaam: TATAKI. Kur 104-128.

Ngaiza, M. K. (2002), "Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study." Unpublished, *Ph.D. Thesis*, UDSM.

Nicholous, A. (2011), "Ubuntu katika Tamthiliya za Penina Mhando," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Njogu, B. na Chimerah, C. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*: Nairobi Jomo Kenyata Foundation.

Nkwera, F. V. (1977), *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Omary, M. (2011), “Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)”, Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ramadhani, D. (2005). *The Uses of Metaphors in Mbogo’s Ngoma ya Ng’wanamalundi and Hussein’s Mashetani. A Stylistic Comparison.*Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa) University of Dar es Salaam.

Ramadhani, S. K. (2013), “Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee”. Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Semzaba, E. (2003). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es salaam. Tanzania. Victoria: Blackwell Publishing.

Sengo, T. S. Y. M. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA.

Senkoro, F. E. M. K, (2006) “Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi simulizi na Fasihi andishi”, katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili chuo kikuu cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Taylor, S. J, na Bogdan, R., (1984), *Introduction to Qualitative Research Methods*. The Search for Meaning. New York: John Wiley & Sons

Wafula, R. M. (2003), *Uhakiki wa Tamthilia Historia na Maendeleo yake*, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi Kenya.

Wamitila, K. W. (2003). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoeni Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Vide - muwa, Nairobi, Kenya.

Young, P. V, (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.